ISSN 2820-2686 | Toleo No. 9 | Oktoba - Desemba | 2023

# JARIDA LA WAKILI MKUU



## *Akaimu Ofisi ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali*

**Ndugu Mark Mulwambo**
**Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Mark Eldad Mulwambo**

Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis Julius Buyekwa**

Afisa Habari

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**

Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**Salome Samuel Magesa**

Kaimu Mkurugenzi wa usuluhishi

**Hangi Matekeleza Chang'a**

Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

**Kiuye Mbwana Shemakame**

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**CPA Devota Mathew Ngulugulu**

Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**

Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**

Mchumi

# TAHARIRI

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ineendelea kuwa kitovu cha kuandaa viongozi wa Serikali hatua ambayo imesaidia ofisi hii kuendelea kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuteua viongozi na kuwakasimu majukumu ya kuendesha baadhi ya taasisi za Serikali na Mahakama ambayo ndio nguzo muhimu ya utoaji haki nchini.

Katika kudhihirisha hilo tarehe 3 Septemba 2023, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya uteuzi wa viongozi mbalimbali kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania kwa lengo la kuuongezea nguvu Mhimili huo muhimu wenye dhamana ya kutoa haki sawa na wakati kwa wananchi.

Pamoja na viongozi walioteuliwa jicho la Mhe. Rais liliiona tena ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kuamua kumteua aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania wakati Tarehe 2 Oktoba, 2023 Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Ndg. George Nathaniel Mandepo kuwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania.

Mafanikio haya makubwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na uongozi thabiti wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambao umekuwa ukisimamia majukumu ya ofisi ambayo ni kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa weledi na uthabiti wa hali ya juu kwa kufuata Sheria, Taratibu na Kanuni za utumishi wa umma.

Kuteuliwa na kuaminiwa kwa viongozi kutoka OWMS kushika nyadhifa hizo muhimu ndani ya nchi ni ishara njema kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa imeweza kuwandaa na kuwajenga watumishi wa OWMS kutekeleza majukumu yao waliyokasimiwa kwa manufaa mapana ya Taifa.

Katika kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na Viongozi Mahiri katika sekta ya sheria na sekta zisizo za kisheria, Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuwaandaa watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya uongozi ili kusaidia kukuza ujuzi na uboebezi katika kasuala ya kiuongozi ili waweze kuwa na uelewa mpana katika uongozi na uwekezaji ili waweze kumsaidia Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa mashauri ya Serikali yanasimamiwa vyema kwa ufanisi na weledi na kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla ili kuendelea kuleta mafanikio makubwa zaidi na kuchangia katika ujenzi wa taifa letu ili kuhakikisha ofisi inaendelea kuandaa viongozi mahiri watakaosaidia kusimamia masuala mbalimbali katika kuhakikisha Serikali inawaletea wananchi wake maendeleo.



**Prisca Jackson Ulomi**
**Mhariri Mkuu**

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



Mark Eldad Mulwambo
**Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Ninayo furaha kubwa kuungana tena na wasomaji wetu wapendwa kwenye Toleo la Tisa la Jarida la Wakili Mkuu. Jarida hili ni Maalumu kwa ajili ya kuangazia majukumu yaliyotekelezwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kwa kipindi cha Mwezi Oktoba hadi Disemba, 2023 ikihusisha uendeshaji wa mashauri mbalimbali yenye maslahi mapana kwa Taifa kama vile uhalali wa uwepo wa Pori la Akiba la Paloleti Wilayani Ngorongoro, ujenzi wa bomba la mafuta na uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam.

Sambamba na kutimiza majukumu yake, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kushiriki warsha ma makongamano mbalimbali kama vile ushiriki kwenye Jukwaa la Majaji Wakuu wa Kusini na Mashariki mwa Afrika, hafla ya kuwaapisha Mawakili wapya waliopokelewa na kukubaliwa na Jaji Mkuu wa Tanzania baada ya kuhitimu masomo kwenye Shule ya Sheria kwa Vitendo (Law School) pamoja na ushiriki katika masuala ya michezo yanayoratibiwa na Shirikisho la Michezo kwa Wizara na Taasisi za Serikali yaliyofanyika mkoani Iringa.

Vile vile, OWMS imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama ya Tanzania na wadau wengine katika kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati.

Sambamba na hayo, Toleo hili litaangazia kwa mara nyingine uteuzi uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua ndugu George Nathaniel Mandepo kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Kabla ya uteuzi huu, ndugu Mandepo alikuwa Mkurugenzi wa Usuluhishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Uteuzi huu unaendelea kuipa heshima Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwa Ofisi inaendelea kuzalisha viongozi wanaoaminiwa na hatimaye kuteuliwa na kukasimiwa majukumu ya kusimamia na kuendesha taasisi mbalimbali za Serikali kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Toleo hili pia litajumuisha makala mbalimbali za kitaluuma zinazotokana na majukumu ya msingi yanayotekelezwa na Ofisi hii kwa lengo la kutoa elimu na kujenga uelewa kuhusu masuala ya kisheria hususan uendeshaji wa mashauri ya madai, usuluhishi, katiba, haki za binadamu na uchaguzi.

Haya ni masuala machache kati ya mengi yatakayoakisiwa kupitia Toleo la Tisa la Jarida la Wakili Mkuu. Naendelea kuwasihi wasomaji wetu kusoma Toleo hili ili kujenga uelewa kuhusu Ofisi inavyotekeleza majukumu yake kwa niaba ya Serikali na kutoa maoni ili kulifanya Jarida hili kuwa chapisho bora. Nawatakia usomaji mwema wa Toleo la Tisa la Jarida la Wakili Mkuu.

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. O6 | Ndugu Mark Eldad Mulwambo Akaimu Ofisi ya Naibu Wakili Mkuu Wa Serikali |
| UK. 07 | Mhe. Dkt. Biteko: Washiriki wa SHIMIWI Tembeleeni Vivutio vya Utalii Vilivyopo nchini |
| UK. 10 | Msuluhishi Hatakuwa na Mamlaka Juu ya Mgogoro Iwapo Hakuna Mkataba wa Usuluhishi |
| UK. 15 | Muswada wa Shehena na Nguvu Yake Kisheria (Bill Of Lading) |
| UK. 20 | Utatuzi wa Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi |
| UK. 22 | Uteuz i na Taarifa kwa Vyombo vya Habari |
| UK. 30 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaanza Kutumia Mfumo wa Manunuzi wa Serikali (NeST) |
| UK. 32 | Prof. Juma: Tumieni Lugha Zisizokiuka Maadili Mahakamani |
| UK. 37 | Mahakama ya Kikatiba Yabariki Uwekezaji katika Bandari Tanzania |
| UK. 41 | Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Yabariki Uwekezaji wa Bomba la Mafuta Ghafi Kutoka Uganda - Tanzania |
| UK. 45 | Serikali Yamaliza Shauri la Dola za Canada Milioni 124,781,945 kwa Majadiliano |
| UK. 45 | Serikali Yamaliza Shauri la Dola za Canada Milioni 124,781,945 kwa Majadiliano |

# NDUGU MARK ELDAD MULWAMBO AKAIMU OFISI YA NAIBU WAKILI MKUU WA SERIKALI

Ndg. Mark Mulwambo amekasimiwa madaraka ya kukaimu nafasi ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali mpaka pale Mamlaka husika itakapoamua vinginevyo baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kumteua Bi. Sarah Duncan Mwaipopo kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania tarehe 03 Septemba, 2023.

Kabla ya kukasimiwa madaraka hayo, ndugu Mulwambo aliongoza Idara ya Madai ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inayojumuisha sehemu ya madai ya ndani, kimataifa, kikatiba, haki za binadamu na uchaguzi.



**NDG. MARK MULWAMBO**

**KAIMU NAIBU WAKILI MKUU WA SERIKALI**



*Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Dotto Biteko (Mb) akizungumza na wanamichezo walioshiriki Mashindano ya SHIMIWI wakati akifungua mashindano hayo yaliyofanyika katika viwanja vya CCM Samora mkoani Iringa.*

# Mhe. Dkt. Biteko: Washiriki wa SHIMIWI Tembeleeni Vivutio vya Utalii Vilivyopo nchini

Wananchi kote nchini hususani wanamichezo wanaoshiriki mashindano ya 37 ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) wamehimizwa kuwa na utamaduni wa kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo nchini hususan mkoani Iringa ili kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Wito huo umetolewa tarehe 4 Oktoba, 2023 na Naibu Waziri Mkuu wa Tanzania na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko (Mb) wakati akifungua rasmi mashindano ya SHIMIWI katika viwanja vya CCM Samora mkoani Iringa.

Dkt. Biteko amesema kuwa kila mwanachi wakiwemo wanamichezo wana kila sababu ya kushiriki kikamilifu katika kutangaza nchi yetu kupitia Sekta ya Utalii huku akitoa pongezi kwa viongozi wa mashindano hayo kwa kuandaa ratiba ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo mkoani Iringa hatua itakayosaidia kuongeza chachu ya ukuaji wa Sekta hiyo nchini.

Mhe. Dkt. Biteko amewahimiza wanamichezo wote wanaoshiriki michezo hiyo kuhakikisha wanashiriki ziara ya kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha inayopatikana mkoani humo ambapo kwa mujibu wa ratiba ya mashindano hayo, wanamichezo hao walitembelea hifadhi hiyo tarehe 07 Oktoba, 2023 ikiwa ni hatua mahsusi ya kutangaza vivutio vya utalii vinavyopatikana nchini kupitia Sekta ya Michezo.

Mhe. Dkt. Biteko ametoa wito kwa wananchi kuwa mstari wa mbele katika kulinda na kutunza mazingira kwa kueleza kuwa athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia ya nchi hazibagui huku akisisitiza kuwa athari hizo zinaweza kuepukika ikiwa kila mmoja wetu kwa nafasi yake atalinda mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yanayotuzunguka.

Amewasisitiza watumishi na wanamichezo kama sehemu ya jamii kuchukua tahadhari zitakazosaidia kujiepusha na shughuli zinazoweza kusababisha ongezeko la mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo kuharibu vyanzo vya maji pamoja na kuteketeza misitu ya asili kote nchini.

Katika hatua nyingine, Mhe. Dkt. Biteko amewataka viongozi wa Wizara na Idara za Serikali kushiriki kikamilifu katika michezo ya SHIMIWI ili kuhamasisha watumishi walio chini yao kushiriki katika michezo hiyo.

Aidha, Mhe. Dkt. Biteko ametumia fursa hiyo kuwapongeza watumishi wote wa Wizara na Idara za Serikali walioshiriki mashindano hayo, na kuwasisitiza kuendelea kushiriki mashindo hayo huku akieleza kuwa michezo ni furaha, michezo huleta umoja, mshikamano na muhimu katika kuimarisha afya za watumishi.

Watumishi kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wameshiriki sherehe za ufunguzi wa mashindano hayo wakiongozwa na Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ndugu Mark Mulwambo, aliyeambatana na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu ndugu James Kimbamba na walishiriki mchezo wa mpira wa miguu kwa wanaume pamoja na kuvuta kamba.



*Timu ya kuvuta kamba ya wanaume ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ikichuana vikali na timu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (haipo pichani) katika mchezo wa kuvuta kamba kwenye mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika mkoani Iringa.*




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakishiriki maandamano ya ufunguzi wa Mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika mkoani Iringa.*




*Timu ya mpira wa miguu ya Wakili Mkuu Sports Club ikiwa katika picha ya pamoja kabla ya mchezo wake na timu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kabla ya kuanza kwa mtanange huo uliofanyika kwenye viwanja vya Chuo cha Mkwawa kilichopo mkoani Iringa.*

# MSULUHISHI HATAKUWA NA MAMLAKA JUU YA MGOGORO IWAPO HAKUNA MKATABA WA USULUHISHI

Mnamo tarehe 2 Septemba 2022, Mahakama Kuu ya Tanzania, Kitengo cha Biashara ilitengua Tuzo ya Msuluhishi kutokana na Msuluhishi kukosa mamlaka ya kimkataba ya kusikiliza na kutoa uamuzi kwenye shauri la Biashara Na. 9 la mwaka 2022 kati ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mengine Tanzania dhidi ya *Monaban Trading & Farming Company Limited*.

Mahakama Kuu ilibaini kuwa Tuzo ya Msuluhishi haina nguvu ya kisheria ili kuweza kutekelezwa Mahakamani hapo kutokana na ukweli kwamba hakukuwa na Makubaliano baina ya wadaawa kuhusu usuluhishi. Mahakama iliamua kuwa, Msuluhishi akikosa mamlaka ya kimkataba ya usuluhishi wa mgogoro husika, chochote anachofanya Msuluhishi huwa ni batili.

Kesi hii ilihusu maombi yaliyowasilishwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Mahakamani kupinga Tuzo ya Msuluhishi kwa vigezo mbalimbali.

Chimbuko la mgogoro huo ni kuwa, mnamo tarehe 23 Agosti 2007, Kampuni ya *Monoban Trading & Farming Co. Ltd*, (Mdaiwa/Mlalamikiwa)



**GEORGE N. MANDEPO**
ALIYEKUWA MKURUGENZI WA USULUHISHI, OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

ilisani Mkataba wa Usagaji wa Mahindi na Ngano na Shirika la Usagishaji la Taifa ("National Miling Corporation - NMC") kwa ajili ya huduma ya usagishaji na uhifadhi katika kiwanda cha mahindi na ngano cha Arusha. Makubaliano hayo yalikuwa ya miaka mitano ambayo yangeweza kuhuishwa kwa kila upande kutoa notisi ya maandishi ya miezi sita kabla ya muda kuisha.

Hata hivyo, tarehe 10 Aprili 2008, pande zote mbili ziliafikiana kuhuisha mkataba huo uliosainiwa mwaka 2007 kwa kuandaa nyongeza ya mkataba ambapo ilidaiwa kuwa, tofauti na makubaliano ya awali, ambayo nia yake ilikuwa kukodisha eneo hilo la kiwanda. Nyongeza hiyo iliyokuwa kinyume cha sheria kwani ilimruhusu mlalamikiwa kupanua uwezo wa kiwanda cha kusaga nafaka kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa dola za kimarekani milioni 2.684. Mkataba huo wa nyongeza uliruhusu mlalamikiwa kulipia gharama za ukarabati na matengenezo ya mitambo kwa NMC chombo ambacho kwa wakati huo kilikuwa kwenye mchakato wa ubinafsishwaji chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC).

Mkataba huo wa ukodishaji ulimalizika mnamo 2013 wakati wahusika waliamua kutoingia upya makubaliano ambapo kwa wakati huo, majukumu ya PSRC yalichukuliwa na Shirikia Hodhi la Mashirika ya Umma (Consolidating Holding Corporation - CHC). Baadaye, kupitia Hati ya uhaulishaji ya tarehe 2 Agosti 2013, Serikali kupitia HAZINA alihamisha baadhi ya mali za iliyokuwa NMC kwenda Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (Mdai/ Mlalamikaji). Miongoni mwa mali hizo ni kiwanja Na.1, 3, 5, 7, 11 na 11A ambacho chini ya Cheti cha Hati Na. 055028/34 kilichopo eneo la Unga Limited, Manispaa ya Arusha, mali inayokuwa kwenye mgogoro baina ya Mlalamikiwa na Mlalamikaji.

## Kufunguliwa kwa Kesi Mahakamani

Tarehe 27 Juni, 2014 mlamikiwa na mlalamikaji walitia saini hati ya mabadiliko ya Mkataba. Tarehe 6 Juni, 2019 mlalamikiwa alikabidhi mali hiyo kwa Serikali na hati ya makabidhiano ilitekelezwa. mlalamikiwa alidai kuwa alikubali kuondolewa kwa mali zake katika majengo hayo ambayo ni pamoja na kiwanda cha kutengeneza mikate na alizeti ifikapo Machi 31, 2020. Hata hivyo, mwaka 2019, mlalamikiwa alifungua shauri Mahakama Kuu, Masijala ya Arusha kati yake na mlalamikaji.

## Kuteuliwa kwa Msuluhishi

Tarehe 31 Machi 2020, Mahakama ilimteua Bi. Christina Ilumba kuwa Msuluhishi kwenye kesi hiyo kutokana na madai kuwa makubaliano ya pande zote mbili yana kifungu cha usuluhishi pindi mgogoro unapotokea. Baada ya kukubaliwa, tarehe 19 Mei, 2020 mlalamikiwa aliwasilisha kwa msuluhishi, hati ya madai kwamba, mgogoro katika usuluhishi huo ulitokana na kitendo cha mlalamikaji kusitisha kwa upande mmoja Mkataba wa Usagaji wa Mahindi na Ngano, na hivyo kupelekea madai hayo. Mlalamikiwa alidai kuwa mlalamikaji alivunja mkataba, hivyo kudai fidia ya kiasi cha shilingi 116,457,592,766.63 na dola za Marekani 151,000,000.

Kwa upande wa mlalamikaji kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipinga madai hayo kwa sababu mbalimbali ikiwemo kutokuwepo kwa mkataba baina ya mlalamikiwa na mlalamikaji unaoweka sharti la usuluhishi. Hata hivyo, msuluhishi baada ya kusikiliza hoja zilizowasilishwa mbele yake, tarehe 2 Aprili 2021, alitoa Tuzo yake ambayo pamoja na mambo mengine aliamuru, na kuelekeza kuwa msuluhishi anayo mamlaka ya kuamua mgogoro kati ya mlalamikaji na mlalamikiwa.

Msuluhishi pia aliamua kuwa Bodi ya Nafaka inapaswa kumlipa fidia mdaiwa kiasi cha shilingi 640,857,800.

## Maombi ya Kupinga Tuzo

Kutokana na kutoridhishwa

na tuzo, Serikali iliwasilisha ombi la kupinga tuzo hiyo na kuomba amri ya kuwa tuzo itenguliwe kwa misingi ya ukiukwaji wa taratibu za usuhishi na msuluhishi kutozingatia mamlaka yake kisheria. Hoja za Serikali zilikuwa kama zifuatavyo:-

(i) Msuluhishi alishughulikia mgogoro uliokuwa mbele yake huku akifahamu wazi kwamba hapakuwa na makubaliano ya usuluhishi yanayompa msuluhishi mamlaka ya kuamua mgogoro na hivyo, tuzo hiyo ilitolewa bila mamlaka yoyote kisheria;

(ii) Msuluhishi alijielekeza vibaya kwa taratibu za kuamua suala hilo huku akijua tangu awali kwamba hakuwa na mamlaka ya kisheria ya kuamua suala hilo;

(iii) Msuluhishi alifanya makosa makubwa kwa kuzingatia kwamba, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko haikurithi Mkataba wa Usagaji, nyongeza yake na Hati ya Tofauti ya NMC inayowekwa wajibu huo chini ya mkataba baina ya NMC iliyofutwa na mlalamikiwa (Monaban).

## Uamuzi wa Mahakamu

Baada ya kuzingatia mawasilisho ya pande zote mbili, Mhe. Jaji Dkt. Nangela ambaye alisikiliza kesi hii aliamua kama ifuatavyo:-

(i) Usuluhishi ni mchakato wa maelewano unaotegemea makubaliano baina ya wahusika kupeleka mgogoro wao kwenye usuluhishi. Kwa sababu wahusika walishindwa kufanya uteuzi, Msuluhishi aliteuliwa na Mahakama kwa mujibu wa kifungu cha 8 (2) cha Sheria ya Usuluhishi kwa wakati huo, Sura ya 15 RE 2019;

(ii) Uteuzi wa msuluhishi uliofanywa na Mahakama, haukumpa msuluhishi mamlaka yake ya kuendelea na usuluhishi wa mgogoro pasipo kujiridhisha kama mamlaka hayo yapo katika mkataba wa usuluhishi baina ya wadaawa. Badala yake, Mahakama ilichofanya ni kumteua msuluhishi ambaye atasimamia suala hilo baada ya pande zote kukubaliana. Pia, msuluhishi huyo alikuwa na wajibu wa kuhakiki kama ana mamlaka ya kulisikiliza shauri husika;

(iii) Katika kifungu cha 34(1)(a) cha Sheria ya Usuluhishi, msuluhishi amepewa mamlaka ya kuamua iwapo kuna makubaliano halali ya usuluhishi. Hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa msingi wa mamlaka ya usuluhishi ni makubaliano halali baina ya pande husika katika mgogoro;

(iv) Wahusika katika mgogoro wanampa mamlaka msuluhishi kwa makubaliano yao ya kutaka usuluhishi ufanyike. Hata kama msuluhishi aliteuliwa na Mahakama, kwa kuwa alipaswa kutoa uamuzi kuhusu uwezo wake kulingana na makubaliano ya usuluhishi, Mahakama haiwezi kuzuiwa kuamua iwapo kulikuwa na changamoto yoyote kuhusu mamlaka ya Msuluhishi;

(v) Msuluhishi alikosa mamlaka ya kutosha kutokana na ukweli kwamba, makubaliano ya usuluhishi na makubaliano ya mkataba yalikuwa batili hivyo, tuzo ya msuluhishi iliyotolewa tarehe 2 Aprili, 2021 ni batili kwa mujibu wa kifungu cha 74(3)(c) cha Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 [RE 2020] mahakama iliitengua tuzo iliyotolewa.

## Umuhimu wa Uamuzi

Uamuzi katika kesi hii ni miongoni mwa maamuzi machache ambayo Mahakama Kuu ya Tanzania kupitia Sheria ya Usuluhishi ya mwaka 2020 iliweza kutengua tuzo ya msuluhishi na kukubaliana na hoja za Serikali kwamba, mamlaka ya kisheria ya msuluhishi ni lazima yawepo kwenye mkataba au makubaliano ya usuluhishi.

Tofauti na aina nyingine za utatuzi wa migogoro ikiwemo Mahakamani, utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala (Alternative Dispute Resolution - ADR), unahitaji la lazima la kuwepo kwa makubaliano yaliyo wazi ya wahusika katika mgogoro kutaka mgogoro wao uamuliwe kwa njia ya usuluhishi. Wahusika wanaweza kuweka masharti katika Mkataba wao wa utaratibu au namna utatuzi utakavyofanyika, muda na taasisi au mtu ambaye

wanaona kuwa anaweza kusaidia katika utatuzi au usuluhishi wa mgogoro wao pindi utakapotokea.

Katika kesi hii, Mahakama ilikubaliana na Serikali kwamba hapakuwa na makubaliano ya usuluhishi baina ya *Monaban Trading & Farming Co. Limited* na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo yangeweza kumpa mamlaka msuluhishi ya kuamua mgogoro huo. Uamuzi huu ulithibitisha umuhimu wa makubaliano ya usuluhishi ambayo chini yake mhusika katika usuluhishi, anapaswa kuanzisha mgogoro na kuupelekea kwa usuluhishi iwapo tu yapo makubaliano ya usuluhishi ili kumpa msuluhishi mamlaka.

Usuluhishi ukiwa ni utaratibu wa kibinafsi wa walio katika mgogoro wa kumaliza tofauti au mgogoro baina yao, unapaswa kuwa ni utaratibu wa hiyari ya pande zote mbili na kwamba kabla ya kupelekea mgogoro kwenye usuluhishi, ni lazima mlalamikaji ajiridhishe kuwepo kwa mkataba wa usuluhishi baina yake na yule anayemlalamikia na kwamba mgogoro upo na utaratibu wa usuluhishi umewekwa kisheria.

Ikumbukwe kwamba, kwa kawaida kuna haki ya moja kwa moja ya kupeleka mgogoro mahakamani, haki ya kwenda kwenye usuluhishi kwa asili yake ina vikwazo. Kuna masharti matatu ambayo yanapaswa yatimizwe kabla ya uamuzi na kesi ya usuluhishi kuanza. masharti ni kama ifuatavyo:-

(i) Lazima kuwe na mgogoro au mgongano wa kweli au tofauti kati ya pande zinazoweza kusuluhishwa au kuamuliwa kupitia tuzo ya msuluhishi/mwamuzi ambayo inaweza kutekelezwa kama hukumu ya mahakama;

(ii) Lazima pawepo na makubaliano ya kimkataba ya kisheria ya usuluhishi au uamuzi ambayo yanaruhusu upande wa makubaliano hayo kuwasilisha mgogoro au tofauti baina yao kwa usuluhishi/hukumu ya mtu wa tatu aliyechaguliwa au aliyeteuliwa kwa mujibu wa maelekezo yao. Makubaliano ya usuluhishi yanaweza kufanywa wakati mgogoro tayari umetokea au yanaweza kuwekwa tangu mwanzo katika mkataba mama;

(iii) Lazima kuwe na uwasilishaji au marejeo ya mgogoro maalum kwa msuluhishi au mwamuzi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa katika makubaliano ya uamuzi au usuluhishi. Utaratibu huo unajumuisha notisi ya kuelekeza mgogoro kwenye usuluhishi.

Masharti ya hapo juu ni muhimu sana kuchunguzwa kwenye kila shauri la usuluhishi ili wale wanaopeleka kesi zao kwenye usuluhishi waweza kupata maamuzi au tuzo inayoweza kuwa na nguvu kisheria ya kukaziwa au kutekelezwa Mahakamani. Vinginevyo, mhusika ambaye hataki kwenda kwenye usuluhishi anaweza kupinga shauri hilo iwapo masharti ya misingi ya kisheria hayajazingatiwa.

Aidha, ili usuluhishi ufanikiwe, ni lazima kuwepo na mgogoro halisi. Iwapo hakuna mgogoro, basi msuluhishi aliyeteuliwa hawezi kuwa na mamlaka ya kuamua jambo alilopelekwa kwa uamuzi.

Kwa Tanzania, Sheria ya Usuluhishi ya Mwaka 2020 Sura ya 15 ya Sheria za Tanzania na Kanuni za Usuluishi Tangazo la Serikali Na. 146 la Mwaka 2021 ndio zinazosimamia taratibu za usuluhishi. Sheria ya Usuluhishi, Sura ya 15 ilitungwa upya mwaka 2020 baada ya kufutwa iliyokuwepo tangu enzi za ukoloni. Sheria hii inaweka masharti ya utatuzi wa migogoro kirafiki nje ya mfumo wa Mahakama pamoja na kuwezesha utekelezaji wa makubaliano ya kiusuluhishi.

Sheria hii inasimamia na kushughulikia masuala mbalimbali yanayotokana na mashauri ya usuluhishi pamoja na kutoa mwongozo unaohusu misingi ya usuluhishi, maana ya usuluhishi na chanzo cha makubaliano ya usuluhishi. Sheria inaweka utaratibu wa utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Usuluhishi ambayo Tanzania Bara imeridhia na kuweka mfumo madhubuti wa usimamizi na uratibu wa usuluhishi.

Pamoja na masuala mengine, Sheria inaratibu masuala mbalimbali ya makubaliano ya usuluhishi ikiwemo kutafsiri makubaliano ya usuluhishi na hatma ya makubaliano iwapo mmoja wa muhusika atafariki; kuanza kwa usuluhishi, uwezo wa Mahakama kuongeza muda wa kuanza kwa usuluhishi na kutumika kwa Sheria ya Ukomo wa Muda, Sura ya 89; uanzishwaji wa Mabaraza ya Usuluhishi ikiwemo uteuzi wa wasuluhishi, mwenyekiti na waamuzi.

Sheria pia inaainisha mamlaka ya Baraza la Usuluhishi na kuweka utaratibu wa kuhoji mamlaka ya Baraza. Aidha, inaweka utaratibu wa kufuatwa pindi mhusika anapodhamiria kuweka pingamizi la awali kuhusu mamlaka ya Baraza. Sheria pia inaweka utaratibu wa mwenendo wa mashauri kwenye Baraza kwa kuainisha wajibu wa Baraza, masuala ya taratibu za ushahidi, uteuzi wa wanasheria au wataalam. Vilevile, inaainisha kuhusu mamlaka ya Baraza na amri ambazo Baraza linaweza kuzitekeleza kwa mhusika aliyeshindwa kutekeleza amri za awali za Baraza hilo na gharama za usuluhishi ikiwemo gharama ambazo zinaweza kufidiwa pamoja na gharama za wasuluhishi na ukomo wa gharama hizo. Sheria imeipatia pia mamlaka ya mahakama kuhusiana na utekelezaji wa tuzo na haki ya rufaa endapo kuna ukiukwaji wa sheria. Aidha, inatoa mwongozo kuhusiana na mhusika ambaye ameshindwa kushiriki katika shauri la usuluhishi na kutoa kinga kwa taasisi za usuluhishi.

Kupitia Sheria hii, Kituo cha Usuluhishi kimeanzishwa kwa lengo la kushughulika usuluhishi wa migogoro ya ndani na nje ya Tanzania Bara. Aidha, Kituo hicho kina mahusiano na vituo vingine vya usuluhishi vya Kimataifa. Sheria pia inaainisha masharti kuhusu utambuzi na utekelezaji wa tuzo zilizotolewa ndani na nje ya nchi. Sehemu hii inatoa pia tafsiri ya tuzo, vigezo na masharti ya utekelezaji wa tuzo hizo pamoja na namna ambavyo Mahakama itatambua Amri mbalimbali zinazotolewa.

# MUSWADA WA SHEHENA NA NGUVU YAKE KISHERIA (BILL OF LADING)

Katika biashara za kimataifa za bahari shehena ya mzigo/bidhaa hutumika kama hati ya kusafirisha bidhaa. Muswada wa shehena ni mkataba kati ya mtumaji wa bidhaa na mtoa huduma ambaye ana jukumu la kuzisafirisha.

Taarifa ya Katibu wa Umoja wa Mataifa katika Masuala ya Biashara na Maendeleo ya Mwaka 1971 (United Nations Conference on Trade and Development (UNCTAD), Aya ya Kwanza, imetafasiri Muswada wa shehena kama "hati inayothibitisha upakiaji wa bidhaa kwenye meli."

Kwa mujibu wa Sheria za Uingereza za Halsbury kama nilivyoisoma kupitia tovuti ya Chuo cha Oxford (https://www.law.ox.ac.uk) inafafanua Muswada wa shehena kama; "Hati iliyotiwa saini na mmiliki, au wakala wa mwenye meli, ambayo inasema kwamba bidhaa fulani zilizoainishwa zimesafirishwa kwa njia fulani, mathalani meli." Kwa maneno mepesi Muswada wa Shehena ni waraka wa kisheria unaotolewa na kampuni ya usafirishaji kwa msafirishaji ambayo huainisha aina, hali na kiasi cha bidhaa au mzigo uliobebwa. Muswada wa shehena kwa kawaida husainiwa na wakala wa upakiaji ikionyesha kiasi na hali ya bidhaa wakati inapakiwa kwenye meli.



SALOME MAGESA

MKURUGENZI MSAIDIZI SEHEMU YA USULUHISHI WA NJE, OFISI WA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Muswada wa shehena mara nyingi husainiwa na wakala wa upakiaji, chini ya muongozo wa taratibu za kisasa. Aidha, wakati mwingine husainiwa na nahodha wa meli kwasababu nahodha ni mwajiriwa wa mwenye meli na anafanya kazi kumwakilisha muajiri wake. Moja ya majukumu ya nahodha wa meli ni pamoja na kuthibitisha wingi au ujazo wa mizigo, kuangalia hali ya mzigo husika unapokuwa tayari kupakiwa kwenye meli.

Athari mahsusi ya kukiri huku ni muhimu zaidi kwa kuzingatia sheria kwamba, meli lazima iwasilishe kile ilichopokea kama ilivyopokea, isipokuwa kama kutatokea majanga

ambayo hayajasababishwa na nahodha au mmiliki wa meli ambapo majanga hayo yanakuwa hayawezi kuepukika kwa mfano tsunami, machafuko au tufani baharini. Hii iliamriwa katika kesi ya *F. C. BRADLEY & SONS, LTD. v. FEDERAL STEAM NAVIGATION CO. (1926) 24 Ll.L.Rep. 446*

Kwa kawaida, Muswada wa Shehena hufanya kazi tatu kuhusiana na suala la upakiaji na usafirishaji wa bidhaa baharini. Hati hii inatumika kama ifuatavyo: -

(i) Risiti ya bidhaa;

(ii) Hatimiliki ya bidhaa; na

(iii) Ushahidi wa mkataba kati ya msafirishaji na mwenye mzigo.

Muswada wa Shehena ya Sheria ya Upakiaji ni hati muhimu katika biashara ya kimataifa na mara nyingi hutumika pamoja na hati nyingine za usafirishaji na forodha na nyaraka hizi kwa pamoja zinaunda msingi wa madai yoyote ya mizigo na mpokeaji ikiwa bidhaa zitawasilishwa kwa muda mfupi au kuharibiwa baada ya kuachiliwa.

Pia, ni msingi wa madai ya mzigo ambapo mnunuzi hukataa hati ya hali, hati ya nyaraka na/au mzigo wenyewe kwa mfano kwenye mkataba wa CIF (*Cost, Insurance and Freight*) ambao bidhaa husika hailingani na maelezo yaliyomo katika ankara ya mauzo. Wakati mwingine, Muswada wa shehena huambatana na alama zilizoandikwa kwenye bidhaa husika. Wakati mwingine bidhaa hizo zinaambatana na maelezo ya hali ya mzigo. Hayo maneno yanaweza kuandikwa na kusomeka kama ifuatavyo "*BIDHAA ILIYO SAFI/ NZURI KATIKA MELI.*" Kwa kimombo (*"CLEAN ON-BOARD BILL OF LADING."*) Hayo maneno yanatumika endapo mzigo uliopakiwa kwenye meli na kupokelewa na nahodha, umethibika kuwa upo katika muonekano na hali nzuri.

**Umuhimu wa Muswada wa Shehena Kwenye Usafirishaji wa Bidhaa Baharini**

**I. Ushahidi wa Mkataba kati ya Msafirishaji na Mbebaji**

Chini ya Sheria ya Kimataifa Ya Usafirishaji wa Bidhaa Kwa Njia Ya Majini (Humburg Rules) ya 1978, aya ya 1(7) ya Sheria hiyo, imeeleza kuwa, muswada wa shehena ni ushahidi wa kimsingi kwamba kiasi cha bidhaa zinazodaiwa kusafirishwa zimesafirishwa. Ili kuepuka kuwajibishwa mtoa huduma au mwenye meli na wajibu wa kuthibitisha kuwa bidhaa zinazodaiwa kusafirishwa, hazikusafirishwa kama ilivyo elezwa katika muswada wa shehena wa sheria ya upakiaji.

Si hivyo tu bali, msafirishaji nae ana wajibu wa kuthibitisha ya kwamba ni kweli mzigo ulisafirishwa pasi na shaka na si vinginevyo.

Katika kesi ya Ecu-Line v. Adelakan Na. 10 NWLR (721) 261 ya (2001) mizigo ilipakiwa kwenye meli ambapo miongoni mwa mizigo hiyo kulikuwa na mashine za aina ya photoplotter, Niva 25, na mashine hizo sambamba na mizigo mingine zilisafirishwa kwenye meli inaitwa "MV-Kagoro". Muswada wa shehena ulitumwa kwa njia ya fax na mrufani (Mkata Rufaa) kwenda kwa mjibu maombi. Lakini muswada wa shehena haukuorodhesha mashine hizo za photoplotter, Miva 25 kama nazo zilisafirishwa sambamba na mizigo mingine iliyotajwa. Mara baada ya mizigo kufika bandarini (Port of discharge) ambapo ni nchini Nigeria, mlalamikaji alipoenda kuchukua mzigo huo, alijulishwa kuwa mashine tajwa hazikuwepo sambamba na mizigo mingine iliyotumwa.

Mrufani alishutumiwa kwa kupoteza mashine na alishtakiwa kwa fidia kwa uvunjaji wa mkataba na uzembe katika Mahakama Kuu ya Shirikisho. Hukumu ilitolewa kwa upande wa mlalamikiwa. Hata hivyo, baada ya kukata rufaa, Mahakama ilisema kwamba mkataba wa usafirishaji wa bidhaa yoyote kwa njia ya bahari lazima uthibitishwe na hati ya usafirishaji ambapo Muswada wa shehena hautaji bidhaa fulani, ni ushahidi wa wazi kwamba hizo hazi kuwekwa ndani ya meli.

Muswada ni ushahidi wa mkataba kati ya msafirishaji na mwenye shehena kwa sababu, mkataba halisi kati ya wawili hao hufanywa kabla ya kutolewa kwa Muswada wa Shehena. Tarehe iliyotiwa saini kwenye Muswada kwa niaba ya mkuu wa meli sio tarehe ambayo bidhaa zilipakiwa au kusafirishwa



kwa meli. Kwa kawaida bidhaa au mizigo inaweza kusafirishwa ndani ya meli na hati ya shehena inafuata baadae hiyo ndiyo sababu kwa nini Muswada wa shehena unaweza kusemwa kuwa una kazi ya ushahidi wa mkataba kati ya wawili hao badala ya mkataba halisi.

Mawasiliano kati ya msafirishaji na mwenye shehena hufanywa kwa mazungumzo ya mdomo kabla ya muswada wa shehena na hata kabla ya mizigo kusafirishwa kwenye meli. Mazungumzo kama hayo yanaweza kufanywa kwa mdomo au kwa njia ya simu wakati wa kukodi meli. Iliamuriwa kwenye kesi maarufu sana ya Ardennes (Wamiliki) [1950] 2 ALL ER 517 ambapo mlalamikaji katika kesi hii aliingia mkataba wa makubaliano na mwenye meli wa kusafirishwa machungwa kutoka Hispania kwenda London, Uingereza. Moja ya makubaliano yalikuwa, mwenye meli hakupaswa kubadili safari (No Deviation) badala yake alipaswa kwenda moja kwa moja London, lengo la mwenye mzigo ikiwa ni kuwahi kufika kwa mzigo kabla ya mabadiliko ya sheria mpya ya masuala ya ushuru ambayo ilikuwa ianze kufanya kazi mnamo tarehe 1, mwezi wa Disemba, mwaka huo. Mwenye meli alikiuka makubaliano hayo na akaamua kuongeza safari nyingine na kisha kuendelea na safari kwenda Londoni, kitu ambacho kilipelekea mwenye mzigo kukutana na rungu la ushuru mpya kwasababu meli ilichelewa kufika kinyume na makubaliano yao. Mahakamani mwenye meli alijitetea kuwa muswada wa shehena haukuwa na kipengele chochote kilichomkataza yeye kuchepuka safari na kwenda safari nyingine kubeba mizigo. Mahakama nayo ilisema kwamba makubaliano yao yalifanyika kabla ya safari na makubaliano yake ni mkataba halali na halisi kati ya msafirishaji na mwenye mzigo hivyo msafirishaji (mwenye meli) alikuwa na wajibu wa kufuata maelezo ya makubaliano kwani muswada wa shehena ni ushahidi tu wa uwepo wa mkataba lakini mkataba wenyewe haswa uliingiwa pale walipofanya makubaliano kabla ya safari.



Hivyo mwenye meli alikutwa na hatia.

**II. Risiti ya Bidhaa**

Hii ina maana kwamba Muswada wa Shehena hufanya kazi kama risiti ya kubeba bidhaa na sio pesa. Hutolewa baada ya kujiridhisha kuwa mzigo umefikishwa kwa mpokeaji kama alivyoahidiwa. Upokeaji wa bidhaa unaonyesha yafuatayo: -

Unaonyesha maelezo ya mzigo au shehena iliyo katika kiasi na ubora uliokubaliwa. Kwa mfano ikiwa shehena hiyo ni shehena ya kontena, basi Muswada wa Sheria ya Upakiaji unaotolewa lazima uwe na maneno kama vile "***IMESEMEKANA KUWA NA***" kwa kiingereza ikimaanisha "***SAID TO CONTAIN***" kwa sababu mwenye meli hajui kilichomo ndani ya kontena ndiyo maana, "inasemekana ina".

Mara nyingi kwa mizigo kama ya makontena ambayo inakuwa imefungwa na kuwekewa stika za usalama na maafisa ushuru sambamba na mwenye mzigo baada ya kukaguliwa hasa muda wa kupakia mizigo, ili mtu ambaye sio muhusika asiweze kufungua. Hivyo, nahodha wa meli huwa hajui ndani ya kontena husika kama kuna mzigo ambao umetajwa kwenye muswada wa shehena. Nahodha wa meli kazi yake ni kuangalia hali ya nje ya muonekano wa kontena alizopokea kuona kama ziko sawasawa na iwapo zina uharibifu wowote ama laa ili aweze kuandaa muswada wa shehena kama makontena yako sawa, nahodha wa meli ataandaa muswada wa shehena unaosoma "***BIDHAA AU MZIGO SAFI NDANI YA MELI***" kwa kiingereza "***CLEAN ON BOARD***".

Vivo hivyo iwapo mzigo uliopokelewa utaonekana una hitilafu kwa muonekano wa nje, mwenye meli ataandaa Muswada wa shehena unaosomeka "***MZIGO WENYE HITILAFU/ MCHAFU NDANI YA MELI***" kwa kiingereza "***DIRTY/CLAUSED BILL OF LADING***".

Lengo la kuandika hivyo, ni kumlinda mwenye meli au nahodha wa meli kama

ikitokea mizigo anayosafirisha kwenye makontena hayo ni mzigo haramu au ambao hauruhusiwi kusafirishwa na ni kinyume na sheria nahodha na mwenye meli hawatakuwa na hatia kwani wao hawajui kinachosafirishwa. Lakini pia nahodha na mwenye meli wanapaswa kuwa makini kuandaa muswada wa shehena wa bidhaa husika kwani wakikosea kuandika japo kuwa ni muonekano wa nje, watakuwa matatani. Mfano mzigo uliopokelewa na nahodha ni ***MZIGO WENYE HITILAFU*** na nahodha kwa uzembe ama vinginevyo akaandika kwenye muswada kuwa bidhaa au mzigo uliopokelewa ni ***MZIGO ULIO SAFI/USIO NA ITILAFU*** hapo mwenye meli kupitia nahodha wake watapaswa kulipa fidia kwa mzigo kwakuwa hitalafu au uharibifu utakuwa umefanyika kwenye meli wakati wa kusafirisha mzigo/mizigo.

**III. Hati ya Umiliki.**

Muswada wa shehena hurejewa kama hati ya umiliki kwa sababu inaonyesha umiliki wa shehena. Hii ina maana kuwa mmiliki wa Muswada atachukuliwa kuwa mmiliki halisi wa shehena hiyo na atakuwa na haki ya kudai shehena au bidhaa kwenye bandari ya kusafirisha.

Aidha, muswada ni dhamana ya fedha. Bili ya shehena inatumika kupata mkopo, mpokeaji au mnunuzi wa bidhaa anaweza kupanga na benki yake kufadhili usafirishaji kwa njia ya barua ya mkopo (Letter of Credit). Baada ya kuwasilisha ombi kwa benki ya mnunuzi basi hati zitatumwa kwa benki ya mtumaji ambayo itaangalia uhalali wa hati na kisha itawasiliana na muuzaji ambaye atapakia bidhaa kwenye meli na kukusanya bili ya shehena kutoka kwa msafirishaji. Benki ya mtumaji itakusanya bili ya Upakiaji kutoka kwa muuzaji baada ya kuthibitisha hati zote na benki ya mnunuzi. Kisha itamlipa muuzaji. Bili ya upakiaji itachukuliwa na benki kama dhamana ya malipo. Bili ya shehena itatumwa kwa benki ya mnunuzi ambayo itashikilia hati hadi malipo yatakapofanyika. Malipo yatatumwa kwa benki za muuzaji na kisha mzunguko utakamilika.

Mbali na majukumu haya, hati ya shehena inaweza pia kutumika kama chombo kinachoweza kujadiliwa (negotiable), kuwezesha kununuliwa, kuuzwa au kuuzwa kwa haki yake yenyewe. Hii inaweza kuwa muhimu hasa katika biashara ya kimataifa, ambapo wahusika wanaweza kuwa katika nchi tofauti na bili ya shehena inaweza kutumika kama njia ya malipo au usalama kwa ajili ya mipango ya ufadhili.

Ikumbukwe kwamba hati miliki inayotolewa na hati ya shehena mara nyingi ni ile ya umiliki. Katika kesi ya Meyerstein dhidi ya Barber Erle (1886) 2 LR 38 (CP) iliamriwa kwamba "*uidhinishaji na uwasilishaji wa bili ya shehena, wakati meli iko baharini, hufanya kazi sawa kabisa na utoaji wa bidhaa zenyewe kwa mkabidhiwa baada ya meli kuwasili ingeweza kufanya*". Hii inaonyesha kuwa uwasilishaji wa hati ya shehena ni zaidi ya kukabidhi au kumiliki bidhaa.

**IV. Hitimisho**

Muswada wa Shehena ya Upakiaji ni hati muhimu ambayo inalinda mtoaji na msafirishaji katika biashara za kimataifa baharini. Muswada huandika maelezo kuhusu usafirishaji na hutumika kama sehemu ya marejeo iwapo kutatokea mgogoro. Muswada unatumika kama ushahidi wa kusafirisha bidhaa kwa meli. Waliohusika katika shughuli yoyote ile wanapaswa kuchukua hatua zote zinazohitajika ili kuhakikisha kuwa wanaelewa madhumuni na muundo wa Muswada wa malipo ili kuhakikisha kwamba maslahi yao yanalindwa ipasavyo.

# UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI

## UTANGULIZI

Moja ya majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ya Serikali kuhusiana na wadau wa maendeleo ndani na nje ya nchi. Katika kutimiza wajibu huo, Ofisi inahusika katika kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa namna ambayo itasaidia shughuli za maendeleo ndani ya nchi kwenda mbele.

Uwekezaji nchini ni moja ya chanzo kikuu cha kukuza uchumi wa Taifa. Hivyo, kwa kutambua umuhimu huo, tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikishirikiana na Wizara na Idara nyingine za Serikali katika kusaidia utatuzi wa migogoro mbalimbali inayogusa nyanja za uchumi. Hii ni sehemu ya jitahada za kuvutia wawekezaji nchini zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Uthabiti wa mifumo ya utoaji haki na ushiriki wa Serikali katika kutatua migogoro inayohusu wawekezaji kwa haraka na kwa gharama ndogo, huchukuliwa na wawekezaji kama ni suluhu njema ya kuwasaidia kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara hapa nchini.

Katika kutekeleza majukumu yake mbali na kuendesha mashauri ya usuluhishi kwenye Mahakama na Mabaraza ndani na nje ya nchi, Ofisi imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kumaliza migogoro iliyofunguliwa dhidi/au na Serikali kwa uharaka na gharama nafuu kupitia majadiliano kwa mashauri ambayo yapo mahakamani na kwenye mabaraza ya usuluhishi na migogoro ambayo iko katika hatua ya awali kabla ya kufikishwa kwenye Mabaraza ya Usuluhishi na Mahakami.

### Faida ya Utatuzi wa Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi

Utatuzi wa migogoro umeweza kuimarisha mahusiano baina ya Serikali na wawekezaji wanaoendelea kuwekeza katika sekta mbalimbali za uchumi. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuhakikisha inazuia uzalishaji wa mashauri kwa kufuatilia kwa umakini viashiria mbalimbali vya migogoro ikiwemo malalamiko ya kuwepo kwa vikwazo au ukiukwaji wa sheria, taratibu na mikataba unaofanywa na baadhi ya taasisi za Serikali. Utatuzi wa migogoro unafanyika kabla au baada ya Serikali kufunguliwa mashtaka.

Kwa miaka sita tangu kuanzishwa kwake, Ofisi imeshiriki katika majadiliano mbalimbali na kuwezesha kutatua migogoro mingi ya uwekezaji. Majadiliano yaliyofanyika yamekuwa na manufaa kwenye maeneo mengi ikiwemo:-

(i) Kupunguza gharama kwa Serikali na wadau kwenye uendeshaji wa mashauri;

(ii) Kurejesha mahusiano mema ya kibiashara baina ya Serikali na wabia katika Sekta ya Uwekezaji na ukuaji wa uchumi;

(iii) Kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali kwenye usimamizi wa majadiliano; na

(iv) Kutoa fursa kwa Serikali kutambua vyanzo vya migogoro na kuweka misingi mizuri ya utatuzi na usimamizi wa migogoro.

### Migogoro Iliyotatuliwa kwa Njia ya Usuluhishi

Baadhi ya migogoro ambayo Ofisi ya Wakili Mkuu wa

Serikali imeweza kushiriki na kutatua kwa maslahi ya Taifa kupitia majadiliano ni kama ifuatayo: -

(i) Mgogoro uliohusu kampuni ya madini duniani ambayo ilikuwa ikiidai Serikali zaidi ya dola za Marekani bilioni tatu kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kurekebisha mfumo wa usimamizi wa Sekta ya Madini ili kulinda rasilimali za Taifa. Kupitia kesi iliofunguliwa kwenye Baraza la Usuluhishi, Serikali ilitarajiwa kupata hasara ya zaidi ya shilingi trilioni saba iwapo kesi ingeendelea na Serikali kushindwa. Hata hivyo, kupitia njia ya majadiliano, mgogoro husika ulimalizika na Serikali kuweza kuokoa fedha ambazo ingeweza kulipa iwapo ingeshindwa kesi hiyo, kuisha kwa mgogoro huo kumewezesha wawekezaji wa kampuni husika kuendelea na uwekezaji nchini na kuingia kwenye ubia wa uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali nchini;

(ii) Kumalizika kwa mgogoro uliohusisha Sekta ya Nishati na mwekezaji kutoka Uingereza ambaye aliingia ubia wa kuwekeza katika mradi wa gesi na mafuta na baadae kuibuka kwa mgogoro ambao ulipelekea kufunguliwa kwa shauri akidai kiasi cha dola za Marekani 72,494,138, na fedha za Tanzania 78,111,197.9 lakini kupitia majadiliano yaliyofanyika, pande zote mbili ziliafikana na Serikali haikulipa fedha yoyote hivyo kuokoa kiasi hicho kikubwa cha fedha iwapo kesi ingeendelea na Serikali kushindwa;

(iii) Kumaliza mgogoro uliohusu ujenzi wa daraja la Tanzanite jijini Dar es Salaam ambapo Mkandarasi aliishtaki Serikali akidai kiasi cha dola za Marekani 7,201,528.51 lakini kupitia majadiliano kiasi cha dola za Marekani 4,518,573.91 ziliokolewa kutoka kwenye madai ya msingi.

(iv) Majadiliano ya kesi iliyohusisha Sekta ya Ardhi ambapo wawekezaji walioshinda tuzo walidai jumla ya dola za Marekani 175,841,177. Hata hivyo, kupitia majadiliano Serikali imeweza kushawishi deni hilo kupungua.

Kama ilivyoelezwa, utatuzi wa migogoro ya uwekezaji kwa njia ya majadiliano yameisaidia Serikali kupunguza gharama ambazo zingejitokeza kutokana na kuendesha mashauri hayo na gharama iwapo Serikali ingeshindwa katika mashauri hayo. Sambamba na kuokoa gharama, kutatua migogoro kwa njia ya majadiliano kunazuia kusimama kwa uwekezaji au miradi mingine ya kimkakati ili kupisha majibizano ya kisheria. Hali ambayo ingepelekea nchi kukosa mapato, na kuharibu taswira ya nchi kwa wawekezaji na kwenye nyanja za kimataifa. Vile vile, utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano umepunguza gharama za kutumia Mawakili wa nje ambapo Serikali ilitumia kiasi kikubwa cha fedha hadi kufikia dola za Marekani 11,000,000 kulipa kampuni ya uwakili.

## Hitimisho

Licha ya jitihada za wazi zinazofanywa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kutatua migogoro hiyo, bado kuna uhitaji mkubwa wa Mawakili wa Serikali pamoja na wadau kutoka taasisi na Sekta za Uwekezaji za Serikali kujengewa uwezo kuhusu Sheria za Uwekezaji na utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano. Hii itasaidia kupunguza migogoro inayotokana na utekelezaji hafifu wa kanuni na miongozo ya mikataba ya uwekezaji, kuruhusu uwekezaji bila ya kufanya tathmini ya uwekezaji na mwekezaji. Sambamba na hayo, itawawezesha Mawakili na wadau kufahamu mambo ya kufanya na kutokufanya wakati wa majadiliano.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

## *MAHAKAMA YA HAKI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI YATUPILIA MBALI PINGAMIZI DHIDI YA MRADI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI KUTOKA HOIMA- UGANDA HADI TANGA-TANZANIA*

### 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mnamo tarehe 29 Novemba, 2023, Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imetoa uamuzi wake ambapo imetupilia mbali pingamizi dhidi ya mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki linalojengwa kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania. Uamuzi huu unatokana na shauri la maombi Namba. 29 la mwaka 2020 lililofunguliwa na *Center for Food and Adequate Living Rights Limited* na wenzake watatu dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Uganda na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

1.2 Katika madai yao, Walalamikaji walidai kwamba Mkataba wa utekelezaji wa Mradi huo wa Bomba la Mafuta unakiuka misingi ya haki za binadamu na utasababisha uharibifu wa mazingira kinyume na Ibara ya 6(2)(d), 7(2) na 8(1)(c) ya Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Mkataba wa Usimamizi wa Ziwa Victoria chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Walalamikaji walifungua shauri dogo la maombi ya kuzuia utekelezaji wa mradi huo katika Mahakama hii.

1.3 Katika utetezi wake, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilibainisha kwamba Mkataba huo wa utekelezaji wa Bomba la Mafuta umezingatia misingi yote ya haki za binadamu ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kina kuhusu athari za mazingira na haki za binadamu zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake na kwamba hakuna athari

zozote zilizobainikwa kufanya mradi kuwa kinyume na Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Mkataba wa Usimamizi wa Ziwa Victoria. ***Hivyo, athari ndogo zilizobainishwa kwenye utafiti uliofanywa ziliwekewa mipango mathubuti ya kuweza kuthibiti athari zake kwa mazingira na haki za binadamu.***

1.4 Sambamba na utetezi huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo iliwakilishwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, iliwasilisha mapingamizi matatu (3) ya kisheria kuhoji mamlaka ya Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kusikiliza shauri hilo. Msingi wa hoja za kisheria ulitokana na kwamba Mkataba unaolalamikiwa kati ya Tanzania na Uganda ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2017 na wakati Ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inataka malalamiko kuhusu jambo lolote dhidi ya nchi mwanachama wa Jumuiya kuwasilishwa Mahakamani ndani ya siku sitini (60) tangu kufanyika kwa jambo husika. ***Hoja hii pia iliungwa mkono na Serikali ya Uganda pamoja na hoja nyingine zilizohusu hati ya madai kutokuthibishwa na Walalamikaji na mamlaka ya Mahakama kusikiliza masuala yanayohusu haki za binadamu***.

## 2.0 UAMUZI WA MAHAKAMA

2.1 Katika uamuzi wake, Mahakama ***imekubaliana na hoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba Mahakama haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kwa kuwa linahusu madai ambayo yalitakiwa kuwasilishwa ndani ya muda wa siku sitini (60) kwa mujibu wa Ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, Mkataba unaolalamikiwa, uliingiwa tarehe 26 Mei, 2017 kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda.***

2.2 ***Mahakama pia imebaini kwamba walalamikaji walikuwa na taarifa hiyo na hawakuchukua hatua zozote za kisheria mpaka walivyofanya hivyo Novemba, 2020 ambayo ilikuwa ni zaidi ya miaka mitatu (3) tangu kuingiwa kwa Mkataba huo. Hivyo, baada ya kujiridhisha kwamba malalamiko hayo yanakiuka matakwa ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama imeyatupilia mbali malalamiko hayo pamoja na shauri husika kwa gharama (dismissed with costs).***

## 3.0 HITIMISHO

3.1 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote za Serikali na wadau wengine ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Uganda na Ofisi ya Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ushirikiano wao katika uendeshaji wa shauri hili. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kufanya kazi kwa weledi, uaminifu na uadilifu katika kutelekeza majukumu yake ya ushauri, uratibu na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na Serikali au dhidi ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali
01 Desemba, 2023



# UTEUZI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya uteuzi wa Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Mhe. Rais Dkt. Samia amemteua ndugu George Nathaniel Mandepo kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania nafasi iliyoachwa wazi na ndugu Griffin Venance Mwakapeje aliyeteuliwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Kabla ya uteuzi huo, Mandepo alikuwa Mkurugenzi wa Usuluhishi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.



**GEORGE N. MANDEPO**

ALIYEKUWA MKURUGENZI WA USULUHISHI, OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Kongole kwako ndugu Mandepo!

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

*Doha*
*02 Oktoba, 2023*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi kama ifuatavyo:

i) Amemteua Bw. George Nathaniel Mandepo kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Kabla ya uteuzi huu Bw. Mandepo alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usuluhishi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Bw. Mandepo anachukua nafasi ya Mhe. Griffin Venance Mwakapeje ambaye aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

ii) Amemteua Dkt. Saudin Jacob Mwakaje kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA). Dkt. Mwakaje ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mjumbe wa Baraza lililomaliza muda wake.

iii) Amemteua Bw. George Daniel Yambesi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) kwa kipindi cha pili.

Uteuzi huu umeanza tarehe 01 Oktoba, 2023.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimuapisha ndugu George Nathaniel Mandepo kuwa Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, kwenye hafla iliyofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam. Picha na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu.*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

## *MAHAKAMA YATOA MAAMUZI KUHUSU UHALALI WA UWEPO WA PORI LA AKIBA LA POLOLETI, WILAYA YA NGORONGORO, ARUSHA*

Mnamo tarehe 19 Septemba, 2023; Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha mbele ya Mhe. Jaji J.C. Tiganga ilitoa uamuzi katika shauri Namba 21 la Mwaka 2022 baina *Ndalamia Partareto Taiwap na Wenzake Wanne (4)* dhidi ya *Waziri wa Maliasili na Utalii & Mwanasheria Mkuu wa Serikali.*

Waleta maombi katika Shauri hili ni wananchi wakazi wa Tarafa za Loliondo na Sale, Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha. Kiini cha mgogoro huu ni madai ya wananchi hao kuondolewa katika eneo lililokuwa Pori Tengefu la Pololeti *(Pololeti Game Controlled Area)* lililoanzishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 421 la tarehe 17 Juni 2022 (**Wildlife Conservation (Pololeti Controlled Area) (Declaration Order), 2022***)* lilitolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Wananchi hao wanadai kuwa walikuwa wamiliki halali wa eneo husika kabla ya kutangazwa kuwa Pori Tengefu mwaka 2022.

Aidha, mnamo tarehe 14 Oktoba, 2022, Pori hilo la Pololeti lilipandishwa hadhi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Pori la Akiba yaani **Wildlife Conservation (Pololeti Game Reserve) (Declaration) Order, 2022** kupitia Tangazo la Serikali Na. 604 la 2022

Katika maombi yao Mahakamani, waleta maombi waliomba Mahakama itoe amri ya kumzuia Waziri wa Maliasili na Utalii kuwaondoa waleta maombi na wakazi wa vijiji 14 kwenye eneo la kilometa za mraba 1,500 zinazotengeneza Pori la Akiba la Pololeti.

Ikumbukwe kuwa tarehe 22 Agosti, 2023; Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha mbele ya Mhe. Jaji D. C. Kamuzora ilitoa uamuzi wake katika maombi Na. 178 ya Mwaka 2022 yaliyofunguliwa na Latan'gamwaki Ndwati na

wenzake 6 wakiomba Mahakama itoe idhini (leave) ya kufungua shauri la kupinga Tamko ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuanzisha Pori la Akiba Pololeti, 2022 (Pololeti Game Reserve Declaration Order) G.N No. 604 of 2022. Mhakama katika uamuzi wake iliamua yafuatayo:

i. Ilitoa idhini (leave) kwa waleta maombi kufungua shauri la kupinga utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022; na
ii. Ilisitisha utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 mpaka usikilizwaji wa kesi ya msingi utakapo kamilika.

Tayari wadai wamefungua maombi ya marejeo ya Kimahakama (judicial review) Na. 18 ya Mwaka 2023 katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Arusha ambayo yako katika hatua ya usikilizwaji.

Katika uamuzi wake, ***Mahakama imetupilia maombi hayo ya waleta maombi na kubainisha kwamba Tangazo Na.421 la mwaka 2022 lililotolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii halipo tena katika macho ya sheria kwa kuwa tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelipandisha hadhi eneo hilo kuwa Pori la Akiba (Game Reserve, GR), kupitia Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 na hivyo hakutakuwa na maamuzi yatakayokuwa na nguvu dhidi ya Tangazo hilo kwa kuwa halipo tena.***
***Aidha, Mahakama katika uchambuzi wa hoja zilizokuwa mbele yake ilibaini kwamba eneo ambapo Pori hilo lipo lilikuwepo tangu mwaka 1951. Hivyo, Vijiji viliposajiliwa vililikuta tayari limeanzishwa kama Pori Tengefu ambalo lilijulikana kama Loliondo Game Controlled Area na hoja kwamba eneo hilo ni ardhi ya kijiji moja kwa moja (exclusive) sio kweli bali vijiji ndivyo vilikuta Pori hilo Tengefu. Hoja nyingine tisa (9) za waleta maombi zilitupiliwa mbali na Mahakama kwa kuwa hazikuwa na mashiko kisheria.***

Maamuzi haya ya Mahakama katika shauri Namba 21 la Mwaka 2022 yakisomwa kwa pamoja na maamuzi katika maombi Na 178 ya Mwaka 2022 yana maana ifuatayo:

(i) Tangazo Na.421 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori Tengefu la Pololeti halipo tena katika macho ya sheria kwa kuwa tayari Rais wa Jamhuri ya

2/3

Muungano wa Tanzania amelipandisha hadhi eneo hilo kuwa Pori la Akiba;

(ii) Mahakama imesitisha utekelezaji Tamko la Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kupitia Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori la Akiba la Pololeti mpaka usikilizwaji wa kesi ya msingi Na. 18 ya Mwaka 2023 utakapo kamilika;

(iii) Usitishwaji wa utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022, unawahusu waleta maombi katika shauri Na. 178 la Mwaka 2022 na haiwahusu watu wengine;

***(iv) Kwa kuwa Tangazo Na. 421 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori Tengefu la Pololeti halipo tena na Mahakama imesitisha utekelezaji wa Tangazo Na. 604 la mwaka 2022 la kuanzisha Pori la Akiba la Pololeti, hali ilivyo kwa sasa (status quo) wakati ukisubiriwa uamuzi wa Mahakama katika kesi ya msingi Na. 18 ya Mwaka 2023 ni kwamba eneo lenye mgogoro linaendelea kuwa Pori Tengefu hali iliyokuwa nayo kabla ya kupandishwa hadhi kuwa Pori la Akiba mpaka Mahakama itakapotoa uamuzi kwenye Shauri la msingi. Kwa msingi huo masharti yote yanayosimamia mapori tengefu yanafuatwa ikiwemo kuomba kibali kwa Mkurugenzi wa Wanyapori ili kulisha mifugo katika eneo la Pori Tengefu kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha Sheria ya Wanyama Pori, Sura ya 283 Juzuu la Marejeo ya 2022.***

(v) Wananchi na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii wanakumbushwa kuzingatia sheria katika utekelezaji wa shughuli zao.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

04 Oktoba, 2023

3/3

# *Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yaanza Kutumia Mfumo wa Manunuzi wa Serikali (NeST)*




**Emil Ntangwa**
Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeanza kutumia Mfumo Mpya wa Manunuzi wa Kielektroniki ujulikanao kama ***National e-Procurement System of Tanzania (NeST)*** hatua ambayo imelenga kurahisisha mchakato wa manunuzi ya Serikali kwa kuleta tija na ufanisi unaostahili.

Akizungumza kuhusu faida za Mfumo huo uliotengenezwa na watanzania Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu Emil Ntangwa amesema kuwa mfumo huo utasaidia kuongeza ufanisi katika kusimamia mchakato wa manunuzi kwa kuwa kupitia mfumo huo taasisi za Serikali zitaweza kupunguza michakato ya manunuzi hatua itakayosaidia michakato ya manunuzi kukamilika kwa wakati.

Aliongeza kuwa ujio wa Mfumo huo mpya wa manunuzi wa Serikali umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za manunuzi kwa kuwa kabla ya kutumia mfumo huo tasisi zililazimika kutumia gharama kubwa katika manunuzi ya vifaa mbalimbali tofauti na sasa ambapo mifumo hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za manunuzi.

Aidha, alisisitiza kuwa mfumo huu pia utasaidia Serikali kubana matumizi kwa kufanya manunuzi kwa bei sawa na bei halisi tofauti na hapo awali ambapo Serikali ilitumia fedha nyingi kwenye manunuzi kutokana na ukweli kuwa gharama zilizokuwa zinaletwa na wazabuni zilikuwa kubwa ukilinganisha na gharama halisi zinazopatikana sokoni.


"*Mfumo wa NeST utazisaidia taasisi kupunguza gharama za manunuzi kwa sababu utachagua mzabuni aliyekidhi vigezo vyote lakini zaidi yule aliyependekeza bei ndogo kuliko wote ndiye atakayepewa zabuni,*" alisisitiza Ntangwa.

Kuhusu uwazi, Ntangwa alisema Mfumo wa NeST umeongeza uwazi katika michakato ya manunuzi kwa kuwa mfumo huo umeongeza uwazi zaidi kati ya taasisi za Serikali na watoa huduma ambapo sasa mzabuni ataweza kufuatilia mchakato wa manunuzi kielektroniki kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa mchakato husika.

Alieleza kuwa Mfumo wa NeST umesaidia kuokoa muda katika kuomba zabuni kiurahisi kwenye taasisi za Serikali, kwa sababu kupitia mfumo huu mtoa huduma anaweza kuomba zabuni akiwa mahali popote pale na zabuni hiyo itafanyiwa kazi kwa wakati mara tu baada ya kupokelewa.

Alieleza kuwa kabla ya kuanza kutumia mfumo huo, watoa huduma walilazimika kuomba zabuni kwa kupeleka maombi moja kwa moja kwenye taasisi, zoezi lililochukua muda mrefu na kuwanyima fursa watoa huduma kuomba zabuni hizo kwa wakati.

Mfumo huo ulianza kufanya kazi tarehe 01 Julai, 2023 ukichukua nafasi ya mfumo wa awali TANePS uliokoma kufanya kazi za manunuzi kwa taasisi tangu tarehe 01 Oktoba, 2023.





## Prof. Ibrahim Hamis Juma
Jaji Mkuu wa Tanzania

# *Prof. Juma: Tumieni Lugha Zisizokiuka Maadili Mahakamani*

Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma amewataka Mawakili kuepuka kutumia lugha zinazokiuka maadili wanapowasilisha hoja zao ndani ya Mahakama huku akikitaka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kuchukua hatua kabla ya majaji kulalamika.

Jaji Mkuu ameyasema hayo tarehe 01 Disemba, 2023 wakati akizungumza kwenye sherehe ya 69 ya mahafali ya kuwakubali na kuwapokea Mawakili wapya wapatao 279, idadi ambayo imejumuisha wanawake 118 na wanaume 161 na kufanya jumla ya Mawakili ambao wamekwisha pokelewa kufikia 11,916 kutoka idadi ya awali ya Mawakili 11,636. Hafla hiyo ilifanyika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es salaam.

Mhe. Prof. Juma ameongeza kuwa Mawakili hao wanapaswa kutumia lugha za staha na weledi kwa kuwa uwakili ni taaluma yenye heshima, vitendo vya kiungwana na kauli sahihi ambapo vyote hivi vinahitaji uadilifu.

Prof. Juma ameleeza kuwa amekuwa akipokea malalamikomengikutokakwa Majaji ambapo malalamiko mengi yamekuwa yakihusu

ukiukwaji wa maadili hasa pale Mawakili wa Kujitegemea wanapowasilisha hoja zao mahakamani kwa kiburi, jeuri na kutumia lugha zisizostahili Mahakamani.

"*Malalamiko mengi yanakiuka kanuni ya 92 ya Kanuni ya Maadili ya Mawakili ambayo ndiyo inayowaongoza, hivyo kujibizana na Jaji au Hakimu unakuwa unakiuka moja kwa moja kanuni hii kwa kuwa Mawakili wanao wajibu wa kuheshimu Mahakama kwa kuwasilisha hoja zao kwa lugha zisizoudhi*". amefafanua Mhe. Jaji Mkuu.

Mhe. Prof. Juma ameeleza kuwa ni vyema Mawakili wote nchini kujiepusha na matumizi ya lugha zisizofaa kwa sababu kitendo kimoja tu cha ukiukwaji wa maadili ambacho pengine kimefanywa na Wakili mmoja tu nchini, kinaweza kuharibu taswira yote ya taaluma ya uwakili nchini Tanzania.

"*Kwenye eneo hili mnatakiwa muwe waangalifu, kitendo chochote cha wakili mmoja nchini kukiuka maadili, kinaweza kuchafua taswira ya soko la ajira la Mawakili wa Tanzania kwasababu siku zote inaweza kutumika kama mfano wa hali ya maadili kwa Mawakili wa Tanzania,*" ameongeza Mhe. Prof. Juma.

Jaji Mkuu ameongeza kuwa katika kipindi hiki ambacho ni Karne ya habari na Teknolojia, chochote kinachofanyika leo kinaweza kusambaa kwa haraka zaidi na kwa muda mfupi kwa hiyo aliwaasa kuwa waangalifu katika eneo la maadili kwasababu ukiukwaji wa maadili unaweza kuwachafua Mawakili na taswira yote ya taaluma Mawakili Tanzania.

Jaji Mkuu Mhe. Prof. Juma amesema kuwa kama ilivyo kwa Majaji na Mahakimu, uwakili ni taaluma inayoheshimika sana hivyo vitendo, kauli na mienendo yote ya taaluma hii inapaswa kuwa ya heshima huku akiwaonya Mawakili nchini




*Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma (wa nne kutoka kushoto) akiwa na jopo la Majaji akipokea heshima kutoka kwa Mawakili wapya waliokubaliwa na kupokelewa kuingia kwenye orodha ya daftari la Mawakili kwenye hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam*

kutoruhusu mihuri yao kutumiwa vibaya kwa kuwa kitendo hicho kitapelekea kwa kiasi kikubwa kupunguza hadhi na heshima ya uwakili nchini.

"*Saini zenu mnazosaini ni heshima, nguvu ya taaluma yetu inatokana na heshima, hivyo jamii ikikosa heshima kwetu inakuwa haina maana, siku zote tuwe na tahadhari kubwa ya kutambua kwamba mamlaka yenu ni makubwa sana,*" alisema Mhe. Prof. Juma.

Kuhusu kanuni za kitaaluma zinazotakiwa kuzingatiwa na Mawakili hao, Mhe. Prof. Juma alisema kuwa kanuni hizo kwa kiasi kikubwa zimesaidia kusafisha taaluma ya Mawakili kwa kuwa sasa kila taaluma duniani inatarajiwa kujidhibiti na kuwadhibiti wanataaluma wake kwenye masuala ya nidhamu kabla chombo au mtu yeyote wa nje kuja kusimamia nidhamu ya taaluma husika.

Katika hatua nyingine, Mhe. Prof. Juma amekitaka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kuchukua hatua stahiki na kudhibiti wanachama wake pale wanapokiuka maadili kuhusu masuala ya nidhamu, hatua ambayo ameeleza kuwa itasaidia kuimarisha taaluma hiyo, tofauti na sasa ambapo chombo cha nidhamu kikichukua hatua dhidi ya Mawakili walioenda kinyume na taaluma hiyo Mawakili hao wamekuwa wakikusanyika kuteteana.

"*Sasa Chama chenyewe kichukue hatua za nidhamu, tumieni mamlaka mliyonayo kujidhibiti wenyewe, tumieni kanuni zenu za uwakili za mwaka 2022 kujidhibiti, ni wajibu wenu kuonyesha nidhamu kwa Mahakama,*" alisema Mhe. Prof. Juma.

Mhe. Prof. Juma aliwataka Mawakili hao kuwa na umakini wa kuchagua Mawakili wa kuwa mfano wa kuigwa. Alisema wakili wa kuigwa siyo lazima awe mwandamizi tu bali wachague yule ambaye atawahamasisha,



*Mwasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi  na jopo lake akipokea heshima kutoka kwa Mawakili wapya waliokubaliwa na kupokelewa kuingia kwenye orodha ya daftari la Mawakili wakati wa hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

kuwafundisha na kuwapa hamasa ya kuendelea katika fani hiyo, kuwapa miongozo na mrejesho wa kazi wanazofanya.

Aidha, aliwataka Mawakili hao kuwa na tabia ya kujisomea vitabu ili kuongeza maarifa na kuweza kufahamu masuala mbalimbali kwani kusoma hakuna ukomo na kwamba haipendezi miongoni mwao kuwepo na wahitimu ambao tangu walipohitimu chuo Kikuu hawajawahi kusoma kitabu hata kimoja.

"Acheni tabia za kukumbatia madesa someni kuongeza maarifa mapya ili muweze kukabiliana na ushindani wa karne ya 21, mambo mengi hivi sasa yapo hata mitandaoni", ameongeza Jaji Mkuu.

Mhe. Jaji Prof. Juma amewataka Mawakili hao na Mawakili wote nchini kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa weledi na juhudi kwani wamekuwa Mawakili baada ya kuonesha uwezo katika hatua mbalimbali za elimu walizopitia ikiwemo sekondari, chuoni, shule ya sheria kwa vitendo, Baraza la Elimu ya Sheria na kusailiwa mbele ya Jaji Mkuu.

Kiongozi huyo amesema, kanuni za maadili ya uwakili zinataka Mawakili wote nchini kuwa na huo uwezo huku akiwataka kujiendeleza kwa kuwa kutokufanya hivyo watashindwa kukabiliana na hali ya mabadiliko ya sasa ya ulimwengu, hali itakayopelekea kuwaacha nyuma na kupoteza uwezo unaozungumzwa kwenye maadili ya taaluma ya sheria nchini.

Pia, Mhe. Jaji Mkuu amewasihi Mawakili hao kuendana na hali ya mabadiliko ya teknolojia ambayo hayawasubiri Mawakili na kuongeza kuwa taaluma ya sheria na Mawakili haiwezi kukwepa mapinduzi ya viwanda ambayo tayari yameshaingia mahakamani.

Ameeleza kuwa tayari Mahakama imeanza kujifunza utaratibu mpya wa kuratibu na kusimamia mashauri mahakamani kwa njia ya mtandao. Mfumo



*Sehemu ya Mawakili wapya wakitoa heshima mara baada ya kukubaliwa na kupokelewa na Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma (hayupo pichani).*

huu ni muhimu sana kwani umechukua nafasi ya mfumo uliokuwepo ambao ulizidiwa, mfumo huu unafaida nyingi, ingawaje zipo changamoto kadhaa ambazo bado zinafanyiwa kazi, huku akieleza kuwa faida zitakazopatikana ni kubwa kuliko changamoto ambazo tunazotumia kuimarisha mfumo huo.

Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi akitoa nasaha zake aliwataka Mawakili hao kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku huku akiwakumbusha kwamba Mawakili ni maofisa wa Mahakama hivyo wamepewa dhamana ya kuisaidia Mahakama katika utoaji haki kwa wakati na usawa kwa wote kwani ni jukumu lao kuhakikisha Mahakama inatenda haki.

Jaji Feleshi aliongeza kuwa kanuni ya 92 ya kanuni za maadili ya Mawakili nchini inayohusu mienendo ya Mawakili, inakataza hujuma kwa Mahakama katika utoaji haki ikiwemo kutoa taarifa za uongo, uzushi na kueleza jambo litakaloipotosha Mahakama katika kufikia maamuzi ambayo yasingefikiwa kama upotoshaji huo usingekuwepo.

Mhe. Jaji Dkt. Feleshi amesema kanuni hizo pia zinakataza Mawakili kutoa maoni ya kesi iliyo mahakamani katika mambo ambayo yanaweza kuathiri matokeo ya kesi husika kwa kuwakumbusha kuwa tasnia ya uwakili ni nyeti, hivyo wanapaswa kuzingatia kanuni na miongozo mbalimbali iliyowekwa pale wanapotekeleza majukumu yao hususan kanuni zote za maadili na mienendo ya kazi.

Kuhusu tuhuma kwa baadhi ya Mawakili wa kujitegemea kujihusisha na vitendo vya rushwa kwa baadhi ya Mawakili hao kuwasaliti wateja wao kwa kupokea rushwa, kutohudhuria mahakamani, kutotunza siri za mteja, kutokuwa na mawasiliano mazuri kati ya wakili na mteja na kutumia mihuri isiyo halali amewataka Mawakili hao kuacha tabia hiyo mara moja huku akisema kuwa watachukua hatua stahiki kwa wale wote watakaogundulika kufanya vitendo hivyo visivyofaa kwa jamii.

Mhe. Jaji Feleshi alisema mabadiliko ya sheria ya Mawakili ya mwaka huu imeeleza kuwa Wakili atakayefanya kazi bila kuwa na sifa ya uwakili atapewa adhabu ya kutozwa faini ya shilingi milioni tano na isiyozidi milioni 20 au kifungo cha mwaka mmoja gerezani mpaka miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

"*Nitumie fursa hii kuwaonya wale wote wanaofanya vitendo hivi ambavyo viko kinyume na utaratibu wa taaluma ya sheria na kuacha mara moja,*" alisema Dkt. Feleshi.

Naye, Rais wa Chama cha wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili Harold Sungusia akizungumza wakati wa hafla hiyo, amesema wako katika oparesheni ya kupambana na Mawakili vishoka katika maeneo yote na kuwaasa Mawakili hao kuzingatia maadili na taratibu kwa kuwa taaluma hiyo inahitaji watendaji wanaojitambua na kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa.

"*Kuwa wakili msomi, siyo matangazo ya majigambo na majivuno kama upepo uvumao, bali ni haki ya mhusika kuipenda kusoma kujitafutia taarifa na maarifa sehemu sahihi, kujielimisha, kujikosoa, kujituma na kushirikiana na Mawakili wengine katika kuboresha tasnia hii,*" alisema Sungusia.

Aliongeza kuwa wanajitahidi kusimamia vyema maadili, udhibiti wa matumizi holela ya mihuli na kuhakikisha mihuli ya Mawakili haighushiwi na kueleza kuwa kama chama wameanzisha Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro ya ndani na nje ya nchi ili kupunguza msongamano wa mashauri Mahakamani.

Katika hafla hiyo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliwakilishwa na Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende.

# *Mahakama ya Kikatiba Yabariki Uwekezaji katika Bandari Tanzania*





**Stanley Kalokola**

Wakili wa Serikali

# UTANGULIZI

Bandari za Tanzania zinasimamiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) chini ya Sheria ya Bandari ya Mwaka 2004. Katika kuendeleza shughuli za bandari, Serikali ina wajibu wa kuvutia wawekezaji katika bandari ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa bandari ili kuongeza pato la Taifa. Katika jitihada ya kuendeleza uwekezaji katika bandari, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Falme ya Dubai ziliingia Mkataba wa Mashirikiano tarehe 25 Oktoba, 2022. Mkataba huu unalenga mashirikiano ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshwaji wa utendaji kazi wa bandari.

Kwa mujibu wa Ibara ya 25(2) ya Mkataba huo, Serikali ya Tanzania na Dubai zilitakiwa ndani siku 30 tangu kusainiwa kwa Mkataba huo kuchukua hatua za kisheria kwa mujibu wa Sheria zao kuhakikisha Mkataba huo unaridhiwa na Bunge au chombo kingine chenye mamlaka hayo. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 Bunge ndio chombo chenye mamlaka ya kuridhia Mkataba wa Kimataifa ambao una masharti ya kuridhiwa. Kwa mujibu wa vigezo hivi viwili, Mkataba wa mashirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai ulitakiwa kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Tanzania.

## Kufunguliwa kwa Shauri

Tarehe 16 Mei, 2023 Serikali iliwasilisha Mkataba wa mashirikiano kati yake na Serikali ya Dubai kwa ajili ya taratibu za kuridhiwa kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania. Tarehe 5 Juni, 2023 Bunge lilitoa wito kwa umma kutoa maoni kabla ya Mkataba huo kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Baada ya mchakato wa maoni ndani ya Kamati ya Bunge kukamilika, Mkataba huo uliwasilishwa mbele ya Bunge kwa kujadiliwa na Wabunge na kuridhiwa. Baada ya kujadiliwa na Wabunge, Mkataba huo uliridhiwa kwa mujibu wa matakwa ya Kikatiba.

Tarehe 23 Juni, 2023 ndugu Alphonce Lusako, Emmanuel Kalikenya Chengula, Raphael Japhet Ngonde na Frank John Nyalus walifungua shauri la Kikatiba katika Mahakama Kuu (Masijala ya Mbeya) dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shauri hilo lililofunguliwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba ya Tanzania lilipangwa mbele ya jopo la Majaji watu wakiongozwa na Mhe. D.B Ndunguru, Ismail Kambona na A.S Kagomba.

Katika uendeshaji wa shauri hilo, upande wa walalamikaji waliwakilishwa na jopo la Mawakili wanne wakiongozwa na Mpale Mpoki, Boniphace Mwabukusi, Philip Mwakilima na Livino Ngalimwitumba. Upande wa Serikali uliwakilishwa na jopo la Mawakili wa Serikali sita wakiongozwa na Bw. Mark Mulwambo, Alice Mtulo, Hangi Chang'a, Edison Mweyunge, Stanley Kalokola na Edwin Webiro. Shauri hili lilisikilizwa katika Mahakama ya wazi.

## Malalamiko katika Shauri

Katika shauri hili walalamikaji walikuwa wanalalamikia Mkataba huo wa mashirikiano kwa hoja tano ambazo ni; Moja; Mkataba wa Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Falme ya Dubai unakinzana na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Sheria nyingine za nchi kwa kuruhusu rasilimali za nchi kuchukuliwa. Mbili; Sheria ya Mamlaka ya nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili Sheria Na. 5 ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohousu Rasilimali na Maliasili za nchi, Sheria Na.6 ya mwaka 2017 zimekiukwa kwani Mkataba unaruhusu bandari ambayo ni maliasili kumilikiwa na wageni. Tatu; kwamba

kwa kuruhusu vyombo vya nje kusikiliza migogoro inayohusu maliasili za Tanzania ni kupoteza uhuru wa Taifa na hivyo ni kinyume na Katiba na Sheria ya Umiliki wa Rasilimali na Maliasili. Nne; Uridhiaji Mkataba uliofanywa na Bunge ulikiuka taratibu za kikatiba na kisheria kwa kutokutoa muda wa kutosha kuwezesha umma kutoa maoni na Tano; Mkataba umekiuka Sheria ya Mikataba ya Tanzania kwa kuwa Serikali ya Falme ya Dubai haina nguvu za kisheria kuweza kuingia katika Mkataba. Aidha, walalamikaji wanadai kwamba Mkataba wa mashirikiano umekiuka Sheria ya Ununuzi ya Umma katika mchakato wa kuipatia zabuni kampuni la DP World kama mwekezaji kwenye bandari kwa niaba ya Serikali ya Falme ya Dubai.

## Utetezi wa Serikali

Katika majibu ya Serikali kuhusu malalamiko ya kuvunjwa kwa Katiba na Sheria za nchi, utetezi wa Serikali ulibainisha kwamba, moja; Mkataba uliongiwa na Serikali ya Tanzania na Dubai unajenga msingi wa mashirikiano na sio mkataba wa uwekezaji unaohusisha moja kwa moja maliasili za nchi. Mikataba ya utekelezaji ndio itahusisha maliasili ambazo kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya nchi kuhusiana na Umiliki wa Rasilimali na Maliasili na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Rasilimali na Maliasili za nchi. Aidha, kwa mujibu wa Mkataba, mikataba ya utekelezaji itasimamiwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania na hivyo hakuna ukiukwaji wa Katiba na Sheria za nchi.

Hoja ya pili ni kwamba Mkataba huo wa mashirikiano una hadhi ya kimataifa na hivyo ni Mkataba wa Kimataifa. Kwa msingi huo Mkataba huo unaosimamiwa na Sheria za Kimataifa hivyo unatakwa la kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Hivyo, Sheria ya Mikataba na Sheria ya Manunuzi ya Umma haiwezi kusimamia Mkataba wa Kimataifa. Hivyo, upatikanaji wa Serikali ya Dubai na kampuni ya DP World haukufuata utaratibu wa Sheria ya Manunuzi na Sheria ya Mikataba kama ambavyo walalamikaji wanadai. Hivyo, dhana ya walalamikaji haiendani na taratibu za uwekezaji unaohusisha mashirikiano ya Serikali mbili.

Kuhusu dhana ya kwamba Serikali ya Dubai sio nchi na kwamba haina uwezo wa kisheria kuingia kwenye Mkataba. Katika hoja hii, msimamo wa Serikali ni kwamba kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Montovideo, Serikali ya Dubai ina sifa za kuwa nchi. Aidha, kwa mujibu wa Umoja wa Falme za Kiarabu za Emirates, ni kweli Serikali ya Dubai ni miongoni mwa Serikali zinazounda Umoja wa Falme za Kiarabu za Emirates ambao Umoja huo unatambulika kama nchi ndani ya Umoja wa Mataifa. Aidha, dhana ya uwezo wa kuingia kwenye Mkataba wa mashirikiano haswa ya uwekezaji kwa Serikali zinazounda Umoja wa Falme za Kiarabu za Emirates unasimamiwa na Katiba ya Umoja wa Falme za Kiarabu za Emirates. Kwa mujibu wa Katiba hiyo, masuala ya uwekezaji si sehemu ya mambo ya Muungano katika Umoja wa Falme za Kiarabu za Emirates na hivyo Serikali zinazounda Falme hiyo zina uwezo kisheria kuweza kuingia katika Mkataba na Serikali yoyote.

Hoja ya tatu ni kwamba Bunge lilizingatia matakwa ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba pamoja na Kanuni ya 108(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023 katika kuwashirikisha wananchi kutoa maoni kabla ya mchakato wa kibunge wa kuridhia Mkataba huo haujakamilika. Suala la mwaliko wa siku moja haliwezi kuwa kinyume na Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba na Kanuni 108(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kuwa hakuna takwa la idadi ya siku lililotajwa katika vifungu hivyo. Aidha, wananchi waliokuwa na nia waliwasilisha maoni kwa kufika kwenye Kamati na wengine waliwasilisha maoni kupitia barua pepe ya Bunge.

## Hukumu ya Mahakama

Baada ya kusikiliza hoja za wadaawa, Mahakama katika hukumu yake Mahakama

ilikubaliana na hoja za Serikali. Mahakama ilibaini mambo yafuatayo katika Hukumu yake:-

Moja; Mkataba uliongiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali za Dubai ni Mkataba wa Kimataifa unaosimamiwa na Sheria za Kimataifa. Hivyo, Mkataba huu wa mashirikiano hausimamiwi na Sheria ya Mikataba ya Tanzania ambayo ni Sheria inayohusika na usimamizi wa Mikataba ya ndani. Mahakama ilibaini pia kwamba Mkataba ulioingiwa unahusu mashirikiano ya kiuchumi na kijamii ambayo si sehemu ya mambo ya muungano yanayosimamiwa na Serikali ya Muungano wa Falme za Kiarabu za Emirates ambayo Serikali ya Dubai inazuiliwa kuingia mikataba. Hivyo, Serikali ya Dubai kwa mujibu wa Katiba ya Muungano wa Falme za Emirates ilikuwa na uwezo wa kisheria kuingia katika Mkataba huu wa mashirikiano na kwamba Sheria ya Mikataba ya Tanzania haiwezi kutumika kwa kuwa huu ni mkataba wa kimataifa.


Mbili; hoja huhusu ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma hususan upatikanaji wa kampuni ya Dubai DP World kutozingatia ushindani. Mahakama imeamua kwamba Mkataba huu ni wa mashirikiano ya kiuchumi na kijamii na hauhusishi manunuzi kwa kuwa unalenga kujenga msingi wa kisheria wa mashirikiano. Suala la manunuzi litafanyika katika Mkataba wa nchi mwenyeji na mikataba ya miradi itayaoingiwa baadae na hivyo Sheria ya Ununuzi wa Umma haiwezi kutumika kwenye Mkataba huu wa Kimataifa. Pia, Mahakama ilibainisha kwamba hata Sheria ya Ununuzi wa Umma inatoa hadhi kubwa kwenye Mikataba ya Kimataifa pale unapokinzana na Sheria ya Ununuzi wa Umma. Hivyo, Sheria ya Manunuzi haiwezi kutumika pale ambapo kuna Mkataba wa Kimataifa.

Tatu; Kuhusu Mkataba kukinzana na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mahakama ilibaini kwamba vifungu vya Mkataba havikinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haswa suala la ubinafshaji wa rasilimali za Umma. Kuhusu utaratibu wa uridhiaji wa Mkataba na Bunge, Mahakama imebaini kwamba mamlaka yake hayawezi kuingilia taratibu za ndani za Bunge na hivyo Mahakama ilijizuia kuvuka mipaka yake.

Nne; kuhusu hoja ya utiaji wa saini na uridhiaji wa Mkataba kukinzana na Sheria ya Mamlaka ya nchi kuhusiana na umiliki wa rasilimali na maliasili sheria na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohousu Rasilimali na Maliasili za nchi, Mahakama ilikubaliana kwamba Mkataba husika unaweka msingi wa mashirikiano na hadhi yake ni Mkataba wa kimataifa ambao hauwezi kupimwa kupitia Sheria za ndani na endapo mapungufu kwenye Mkataba hayabatilishi Mkataba kwani yanaweza kurekebishwa kupitia utaratibu uliowekwa kwenye Mkataba.





# Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Yabariki Uwekezaji wa Bomba la Mafuta Ghafi Kutoka Uganda - Tanzania

**Na Stanley Kalokola**
*Wakili wa Serikali*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kutimiza wajibu wake wa kuiwakilisha vyema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mashauri ya madai na usuluhishi. Katika kutimiza wajibu wake, Ofisi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kulinda uwekezaji wa ndani na nje kupitia kuiwakilisha na kushinda mashauri yanayopinga uwekezaji. Makala hii inaangazia uamuzi wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika shauri lililokuwa linapinga uwekezaji katika mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda mpaka Chongoleani mkoani Tanga. Pia, makala inaangazia nafasi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika mashauri yanayohusu uwekezaji.

## Chimbuko la Mradi

Mnamo tarehe 26 Mei 2017 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda ziliingia katika makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) linalojengwa kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania. Mradi huu ambao unatekelezwa katika kilomita 1443, takribani asilimia 80 ambazo ni sawa na kilomita nyingine 1,147 za bomba litajengwa upande wa Tanzania. Mradi huu una thamani ya takribani dola za Marekani bilioni 5.6 ambazo ni sawa na takribani shilingi trilioni 14 za Kitanzania. Mradi huu unatokana na mafuta yanayozalishwa nchini Uganda katika eneo la Ziwa Albert yatakayosafirishwa nchini Tanzania kupitia bomba Pwani ya Bandari ya Tanga na mafuta hayo yatauzwa katika soko la kimataifa. Uzalishaji wa mafuta hayo unatarajia kuanza mwaka 2025.

Muundo wa kisheria na kibiashara wa EACOP ulianzishwa katika Mkataba wa nchi Hodhi uliosainiwa tarehe 11 Aprili 2021 na Terehe 20 Mei 2021 baina ya Kampuni ya EACOP na Serikali za Uganda na Tanzania mtawalia. Aidha, mikataba hiyo iliweka misingi ya mahusiano baina ya Kampuni EACOP na nchi hodhi kuhusu masuala ya ardhi, afya, jamii, usalama, viwango, haki za binadamu, fursa kwa wazawa, usimamizi wa fedha, uidhinishaji na usuluhishaji wa migogoro. Katika utekelezaji wake, bomba linahitaji mkuza wenye upana wa mita 30, sawa sawa na miradi mingine inayotumia muundo wa mstari kama barabara, reli au njia za umeme. Bomba litakalojengwa litakuwa na uwezo wa kutunza joto na litafukiwa chini ya ardhi baada ya ujenzi wake kukamilika. Aidha, udongo wa juu na uoto utarudishwa katika hali yake ya asili na ardhi itakuwa wazi kutumika na watu pamoja na wanyama.

## Kufunguliwa kwa Shauri katika Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

Ni baada ya kusainiwa kwa Mkataba huu wa uwekezaji kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Uganda Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipokea shauri la kupinga mradi huo. Shauri hili lilifunguliwa tarehe 13 Novemba, 2020 dhidi ya Serikali ya Tanzania, Serikali ya Uganda kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Tanzania na Uganda pamoja na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Shauri hili lilifunguliwa na Asasi za Kiraia kutoka nchini Uganda, Kenya na Tanzania wakiongozwa na *Center for Food and Aqeduate Living Rights Limited (CEFROHT), Africa Instutute for Energy Governance (AFIEGO), Natural Justice-Kenya & Center for Strategic Litigation Limited.* Aidha, Wadai walifungua Shauri la Maombi Na. 29/2020 na kuomba Mahakama itoe amri ya kuzuia ujenzi huo hadi Shauri la Msingi Na. 39/2020 litakaposikilizwa.

Msingi wa madai ulikuwa ni utekelezaji wa mradi huu kuwa haujazingatia athari za kimazingira na haki za binadamu kabla ya kutiliwa saini kwa Mkataba wa mashirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda. Pia, wadai walihusisha hoja hizo na madai ya kutolipwa fidia kwa waguswa kutofanyika kwa tathimini ya athari za kimazingira hususani maeneo ya Ziwa Viktoria, mito, misitu na tathimini ya athari za haki za binadamu

na hivyo kufanya mradi kuonekana kuwa unakinzana na matakwa ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 1999. Hivyo, wadai waliomba Mahakama kubatilisha utekelezaji wa mradi huo kwa kile kilichodaiwa kuwa na athari kubwa za mazingira katika eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki kinyume na Ibara ya 6(2)(d), 7(2) na 8(1)(c) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Mkataba wa Usimamizi wa Ziwa Victoria chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, walalamikaji walifungua shauri dogo la maombi ya kuzuia utekelezaji wa mradi huo katika Mahakama hii.

## Utetezi wa Serikali

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilibainisha kwamba Mkataba huo wa utekelezaji wa Bomba la Mafuta Ghafi umezingatia misingi yote ya haki za binadamu ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa kina kuhusu athari za mazingira na haki za binadamu zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake na kwamba hakuna athari zozote zilizobainika kufanya mradi kuwa kinyume na Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Mkataba wa Usimamizi wa Ziwa Viktoria. Serikali iliwasilisha ushahidi wa tafiti za kina za mazingira na haki za binadamu zilizofanyika kabla ya utekelezaji wa mradi.

Hivyo, athari ndogo zilizobainishwa kwenye utafiti uliofanywa ziliwekewa mipango mathubuti ya kuweza kuthibiti athari zake kwa mazingira na haki za binadamu. Pia, utetezi ulibainisha faida zitakazotokana na utekelezaji wa mradi huo kwa nchi husika na kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na fidia na kujengewa nyumba za kisasa kwa waguswa wote, ajira kwa vijana katika eneo lote ambalo ujenzi wa bomba utafanyika, Serikali kujipatia kodi kupata uwekezaji huo pamoja na faida nyingine.

Sambamba na utetezi huo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwasilisha mapingamizi matatu ya kisheria kuhoji mamlaka ya Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuweza kusikiliza shauri hilo. Hoja hizo zilikuwa zinahoji mamlaka ya Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kusikiliza shauri lenye madai yanayohusu uvunjaji wa Haki za Binadamu wakati hakuna Mkataba wa Nyongeza chini ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unaoipa Mahakama mamlaka ya kusikiliza mashauri yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu kwa mujibu wa Ibara ya 27(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hoja nyingine inayohusu muda wa kuwasilisha malalamiko katika Mahakama. Hoja inatokana na takwa la Ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inayotaka malalamiko yote kuwasilishwa ndani ya muda wa siku sitini (60) tangu kutokea kwa tukio husika. Msingi wa hoja hii unatokana na kwamba Mkataba unaolalamikiwa kati ya Tanzania na Uganda ulisainiwa tarehe 26 Mei, 2017 na malalamiko kuhusu Mkataba huo yaliwasilishwa Mahakamani tarehe 13 Novemba, 2020 ikiwa ni zaidi ya miaka mitatu tangu kusainiwa kwa Mkataba huo. Hoja ya mwisho ilihusu hati ya madai kutokuthibitishwa na Mawakili wa taasisi zilizofungua Shauri hilo kwa mujibu wa Kanuni ya 46 ya Kanuni za Uendeshaji wa Mashauri katika Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki za Mwaka 2019.

## Usikilizaji na Uamuzi wa Mahakama

Usikilizaji wa shauri hili ulifanyika kwa njia ya maandishi na mdomo ambapo kila upande ulitakiwa kuwasilisha hoja za maandishi kwanza na baadae kufanya ufafanuzi wa hoja hizo kwa njia ya mdomo. Shauri hili lilisikilizwa mbele ya jopo la Majaji watano kutoka Jumuiya yaAfrika Mashariki wakiongozwa na Mhe. Jaji Yohane B. Massara (Jaji Kiongozi), Jaji Charles O. Nyawello (Makamu Jaji Kiongozi), Jaji Richard Muhumuza, Jaji Richard Wabwire na Jaji Leonard Gacuko. Katika kuendesha shauri hili, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

iliongozwa na Dkt. Boniphace Luhende (Wakili Mkuu wa Serikali), ndugu Mark Mulwambo (Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali), Hangi Chang'a na Viviani Method (Mawakili wa Serikali Wakuu) pamoja na ndugu Stanley Kalokola (Wakili wa Serikali).

Katika uamuzi wake, Mahakama ilikubaliana na hoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mahakama haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kwa kuwa linahusu madai ambayo yalitakiwa kuwasilishwa ndani ya muda wa siku sitini kwa mujibu wa Ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, Mkataba unaolalamikiwa, uliingiwa tarehe 26 Mei, 2017 kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda. Mahakama ilibaini kwamba walalamikaji walikuwa na taarifa hiyo na hawakuchukua hatua yoyote ya kisheria mpaka walivyofanya hivyo tarehe 13 Novemba, 2020 ambayo ilikuwa ni zaidi ya miaka mitatu tangu kuingiwa kwa Mkataba huo. Hivyo, baada ya kujiridhisha kwamba malalamiko hayo yanakiuka matakwa ya Ibara ya 30(2) ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama iliyatupilia mbali malalamiko hayo.

## Nafasi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Kupitia shauri hili, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imejitanabaisha kuwa kinara katika kulinda jitihada za Serikali katika kuchochea uwekezaji ndani ya nchi. Ni dhahiri kuwa uamuzi huu wa Mahakama unaokoa mradi wa zaidi ya dola za Marekani bilioni 5.6 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 14 za kitanzania. Uwekezaji huu ungeweza kupotea kama Serikali ya Tanzania ingeshindwa kwenye shauri hili, hivyo Serikali ingepoteza fursa nyingi za kiuchumi zinazotokana na mradi huu kama kodi, tozo mbalimbali na ajira.

Ofisi imeweza kuzuia hasara kwa Serikali na mwekezaji ambazo zingetokana na aidha kusimamishwa au kufutwa kabisa kwa mradi. Hii ni kutokana na kwamba wakati shauri linafunguliwa tayari Serikali pamoja na mwekezaji walikuwa wametumia gharama nyingi katika kufanya tathmini mbalimbali za mazingira na haki za binadamu, tathimini za fidia kwa waguswa na hatua nyingine za uwekezaji katika mradi huo. Pia, Serikali ingeweza kupoteza fursa za uendelezaji wa bandari ya Tanga ambapo mradi huu utaitumia katika kusafirisha mafuta hayo kwenda kwenye soko la dunia. Hivyo, ushindi huu ni ishara kubwa kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza kulinda uwekezaji na inazingatia masharti ya uwekezaji kabla ya kusaini mikataba hiyo.

Ofisi imeipunguzia Serikali gharama ya kutumia Mawakili binafsi katika kuendesha shauri hili haswa ukizingatiwa kwamba shauri hili limefunguliwa katika Mahakama ya Kimataifa. Uendeshaji wa shauri hili ni jambo kubwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwajengea uwezo Mawakili katika uendeshaji wa mashauri yanayofunguliwa katika Mahakama za Kimataifa.



ICSID International Centre for Settlement of Investment Disputes WORLD BANK GROUP



# Serikali Yamaliza Shauri la Dola za Canada Milioni 124,781,945 kwa Majadiliano




**Na Neisha Shao**
*Wakili wa Serikali*

Tarehe 01 Julai, 2020 Kampuni ya Winshear Gold Corp (Mdai) yenye usajili wake nchini Canada iliishtaki Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Baraza la ICSID kufuatia Serikali kufuta Leseni Hodhi zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni hiyo, kupitia Marekebisho ya Sheria za Madini yaliyofanyika mwaka 2017 na Kanuni za Haki Madini zilizotungwa mwaka 2018.

Madai ya Winshear yaliwasilishwa chini ya Mkataba wa Kulinda Uwekezaji kati ya nchi za Canada na Tanzania. Katika madai yake, Winshear ilidai kuwa Serikali imekiuka makubaliano ya uwekezaji kwa kutaifisha uwekezaji wake kupitia Kampuni ya Tanzania ya Bafex Tanzania Limited bila kufuata taratibu na kuilipa kampuni hiyo fidia stahiki. Pia, ilidai kuwa Serikali haikutoa haki na usawa kwa wawekezaji chini ya mkataba wa uwekezaji kati ya Canada na Tanzania. Hivyo, Kampuni iliwasilisha madai yake katika baraza la ICSID tarehe tarehe 2 Julai 2021 ikiomba baraza hilo kutoa amri kuwa Serikali ya Tanzania imetaifisha uwekezaji wa Kampuni yake na kuomba kulipwa fidia ya kiasi cha dola za Canada 124,781,945.

Mdai aliwakilishwa na Kampuni ya Mawakili ya LALIVE ya nchini Uswizi na Kampuni ya Boies Schiller Flexner (UK) LLP ya nchini Uingereza wakati upande wa Serikali uliwakilishwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Kabla ya kusikilizwa kwa shauri hili, pande zote mbili ziliwasilisha mawasilisho na nyaraka mbalimbali kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili. Katika kuwasilisha nyaraka hizo, pande zote mbili zilifanikiwa kuwasilisha Madai ya Wadai (Memorial), Utetezi wa Serikali (Counter Memorial), majibu ya nyongeza ya Wadai (Claimant's Reply) na Majibu ya nyongeza ya Serikali (Respondent's Rejoinder). Pia, pande zote mbili zilikuwa na jumla ya mashahidi sita, vielelezo vya ushahidi 529, vielezo vya kisheria 179, na vielelezo vya mtaalam 117.

Shauri hili lilisikilizwa kuanzia tarehe 13- 17 Februari, 2023 mbele ya wasuluhishi Prof. Gabrielle Kaufmann-Kohler (Rais wa baraza), Jaji Thomas Johnson, na ndugu Edward William Fashole Luke II. Hata hivyo kabla ya kusikilizwa kwa shauri hili, Serikali ilianza mazungumzo na mdai ya kusuluhisha shauri hili nje ya usuluhishi. Baada ya mazungumzo ya takribani mwaka mmoja tarehe 6 Oktoba, 2023 pande zote zilitia saini hati ya kumaliza mgogoro huu nje ya Mahakama kwa Serikali kulipa wadai kiasi cha dola za Marekani millioni 30.

Shauri hili ni moja ya mashauri makubwa yenye madai ya mamilioni ya dola za Marekani yaliyomalizwa kwa njia ya majadiliano na wadai kukubali kupunguza kiasi kikubwa cha fedha jambo liloiwezesha Serikali kuokoa kiasi cha dola za Marekani milioni 59,843,000.4 kwa njia ya majadiliano.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa ikizingatia mambo yafuatayo ili kuhakikisha inafanikiwa kwenye majadiliano. Kwanza; kuainisha shauri kwa undani na kujua nguvu na mapungufu ya shauri kwa pande zote. Ni muhimu kabla ya majadiliano kuelewa kesi kwa undani na kuainisha maeneo ambayo yananguvu kwa upande wako pamoja na mapungufu ili kuweza kuelewa maeneo gani ya kuanza nayo na yapi yanahitaji mkazo zaidi au la!. Pili; kusikiliza kwa umakini. Ni muhimu kuwa na nyenzo stahiki za kusikiliza ili kuweza kufanya majadiliano yenye manufaa. Unaposikiliza kuna uwezekano mkubwa kuelewa mawazo ya upande wa pili kabla ya kuanza mazungumzo Tatu; kupanga mambo ya kutekeleza na kujiwekea muda wa kutekeleza. Baadhi ya mazungumzo hutumia zaidi ya miaka mitano, ila ili mazungumzo yawe yenye tija ni vyema kupanga vitu vinavyotakiwa kufanyika na pande zote na kujiwekea muda wa kutekeleza. Nne; kuwa na lengo. Ili majadiliano yafanikiwe ni muhimu kuwa na lengo ambalo unataka kulifikia. Lengo hili huwa kama ramani itakayosaidia kuongoza majadiliano. Tano; fanya utafiti. Ni muhimu kufanya utafiti yakinifu kabla ya kuanza majadiliano. Fahamu shauri lako kwa undani na kuwa na taarifa zote ambazo zitasaidia katika kuielewa kesi kwa undani pamoja na upande wa pili. Hii itarahisisha majadiliano.

Haya ni baadhi ya mambo ya kuzingatia ili kufanikisha majadiliano, weledi na kuweka maslahi mapana ya taifa pale tunapofanya majadiliano yoyote ili kuweza kulinda rasilimali zetu.

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |